# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Agosti 27, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580321

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Uteuzi urais NEC wamkwamisha Tundu Lissu kufika mahakamani

UKURASA 4



ama

AFYA NA MAZINGIRA

Wanawake waeleza athari janga la corona

Taathiri ya ubakaji ilivyochangia kumletea ugumba binti miaka14

Chunga, kucheua ni hatari afya ya koo kwa watu wazima

MAZINGIRA

KUDHIBITI TABIANCHI

• Mitungi gesi kilo 2 yafika vijijini • Gesi asilia yasambazwa pia

Mfano mtungi wa kilo 28 ni Sh. 50,000 bei yake hajjab-adilika kwa muda mrefu na hata ukija Dodoma uta-kuta bei ni hiyo hiyo, ndiyo maana hailsi ya bei nafuu.

UKURASA 22

# SARAKASI

• **Moto** sasa wawaka kwenye mapingamizi, NEC yazuia kujitangaza kupita bila kupingwa... *Endelea ukurasa 2*



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipokea fomu ya kuomba uteuzi wa nafasi hiyo kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud Hamid mjini Zanzibar jana.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia AFP, Said Soud, akipokea fomu ya kuomba uteuzi wa kugombea nafasi hiyo, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, mjini Zanzibar jana. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMAN**

## Mwinyi, Soud waahidi makubwa Zanzibar

UKURASA 3

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**KORTI YA MAFISADI YAHUKUMU KINA KITILYA KULIPA MABILIONI**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu...

UKURASA WA 5

**TCU YAFUNGUA DIRISHA MAOMBI VYUO VIKUU**

TUME ya Vyuo Vikuu (TCU), imefungua dirisha la maombi ya udahili wa...


## CUF kuanzia kampeni Mtwara

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nziku, akikagua gwaride lililoandaliwa na Jeshi Usu la Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), baada ya kutembelea makao makuu ya mamlaka hiyo, Kingolwira, mkoani Morogoro jana. **PICHA: TAWA**

# Sarakasi za ubunge zazidi kunoga

**Na Waandishi Wetu**

NI sarakasi. Ndivyo inavyoonekana kutokana na vitimbi na mambo yanayoendelea katika majimbo kwenye nafasi za ubunge na udiwani.

Hiyo ni baada ya taarifa kutoka sehemu mbalimbali kueleza kuwa baadhi ya wagombea wa vyama wamekatwa na wasimamizi kugombea nafasi hizo na wengine kudaiwa kuvamiwa na kupokonywa fomu kabla hawajazirejesha.

Hatua hiyo imesababisha baadhi ya vyama ambavyo wagombea wao wametangazwa kukatwa kwa kutokukidhi vigezo vilivyowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutoa matamko mazito.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa kauli nzito kwamba baada ya NEC kuwapitisha Tundu Lissu na Salum Mwalimu kuwa mgombea urais na mgombea mwenza, sasa kinaelekeza nguvu zake kukabiliana na mapingamizi waliowekewa wabunge wake katika baadhi ya majimbo nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa CHADEMA, Tumaini Makene, aliiambia Nipashe jana kuwa wanaendelea na kazi ya kuweka pingamizi na kukata rufani maeneo ambayo wagombea ubunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamedaiwa kupita bila kupingwa.

"Hatua inayofuata ni kukabiliana na pingamizi na sisi kuwawekea pingamizi na kukata rufaa (rufani) maeneo yote ambayo CCM kupitia hujuma za wasimamizi, uoga na hofu ya uchaguzi, walilazimisha wapite bila kupingwa," alisema Makene.

Alisema utekelezaji wa mkakati huo ulianza jana kwa kwenda ofisi za NEC kwa ajili ya kuweka pingamizi na kukata rufani. Hadi kufika jana, majimbo 18 yalidaiwa kuwa wagombea wa CCM walitangazwa kupita bila kupingwa kutokana na wagombea wa vyama vingine kuwa na kasoro mbalimbali zilizowafanya kutosimamishwa na NEC kuwania nafasi za ubunge.

Majimbo hayo ni Misungwi, Ruangwa, Ushetu, Morogoro Mjini, Morogoro Kusini, Mvomero, Kilosa, Mtama, Gairo, Kongwa, Chamwino, Namtumbo, Kavuu, Katavi, Kondoa, Mpwapwa, Vwawa na Dodoma Mjini.

**ACT-WAZALENDO YALONGA**

Wakati CHADEMA ikitoa msimamo huo, Chama cha ACT-WAZALENDO kimeiomba NEC kushughulikia changamoto mbalimbali zilizojitokeza kwenye mchakato wa urudishwaji fomu za ubunge na udiwani kwenye maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo wagombea kutokupewa fomu na kunyimwa fomu za mapingamizi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meneja Kampeni wa Chama hicho, Emmanuel Mvula, amesema kuna baadhi ya maeneo waliyobaini changamoto zilizosababisha wasimamizi wa uchaguzi kushindwa kuzitatua. Alisema hatua hiyo ilisababisha taharuki kwa wagombea wao baada ya majina yao kuondolewa kwenye uteuzi.

"Kumekuwapo na ukiukwaji mkubwa wa sheria na kanuni za uteuzi katika baadhi ya majimbo na kata na kusababisha wagombea kukosa fomu za uteuzi sambamba na za mapingamizi," alisema Mvula.

Alisisitiza kuwa chama hicho kitaendelea kusisitiza kufanyika uchaguzi kwa utulivu na amani huku ikitaka NEC kushughulikia mapingamizi yote ya wagombea wao na kuwateua ili kuwapa fursa wananchi kuchagua viongozi wanaowataka.

"Tutaweka mapingamizi kwa wagombea wote waliopita bila kupingwa au bila kuwa na mshindani kwa sababu tunaamini hawajawafanyia hivyo kwa uhalali na tunaamini tume itasikiliza mapingamizi yetu," alisema.

Mvula pia alisema yako matukio yaliyojitokeza ya wagombea wa chama hicho kuporwa fomu, kutekwa na watu wasiojulikana na wengine kukamatwa na polisi katika baadhi ya majimbo na kata, madai ambayo pia yameshatolewa na CHADEMA.

**ATINGA 'KININJA' KUREJESHA FOMU**

Katika hali isiyotarajiwa, baadhi ya wagombea ubunge wameibuka na mbinu mpya za kukabiliana na watu wasiojulikana ambao wamekuwa wakiwavamia na kuwapora fomu hizo.

Mgombea ubunge Jimbo la Pangani kupitia ACT-Wazalendo, Faraji Msagati, juzi alitinga kwa Msimamizi wa Uchaguzi akiwa amevaa vazi la mwanamke, maarufu kama Ninja, lililofunika uso wake.

Msagati alikwenda kuwasilisha pingamizi dhidi ya mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Jumaa Aweso na kuwasilisha majibu ya pingamizi alilowekewa.

Mgombea huyo amelazimika kufanya hivyo kwa lengo la kuwakwepa watu aliodai kuwa ni maofisa Uhamiaji.

Naye mgombea ubunge Jimbo la Misungwi kupitia CHADEMA, Mwalimu Shija Samweli, alieleza alivyoficha fomu zake kwenye shati alilokuwa amevaa ili kukabiliana na watu hao wasiojuliana.

Katika video fupi iliyosambaa mtandaoni, Samweli alisema alilazimika kuvaa koti lenye kofia kwa sababu alijua kuna mazingira yanaweza kutokea baada ya kufeli kila mbinu waliyokuwa wakifanya.

"Walichana koti langu na kuniibia fomu, lakini waliyokimbia nayo ilikuwa bandia na fomu halisi niliiweka kwenye shati nililolivaa na kuvaa kikoti ili kusaidia," alisema.

■**Imeandikwa na Romana Mallya, Mary Geofrey na Enock Charles.**

## NEC yazuia kujitangaza kushinda bila kupingwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetolea ufafanuzi dosari iliyojitokeza katika mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu kwa baadhi ya wagombea kutangazwa kupita bila kupingwa.

Vilevile, imebainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa kutokana na baadhi ya wagombea kuenguliwa kwa madai ya kutokukidhi sifa na masharti ya uteuzi.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema tume inafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu hivyo hakuna mgombea atakayekatwa kwa matakwa fulani.

"Kuna taarifa mitandaoni watu wakilalamika kukatwa, suala la uteuzi mtu hawezi kukatwa kwa matakwa ya mtu. Tume inafanya kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni.

"Tumeweka kabisa sifa za wagombea katika ngazi zote za madiwani, wabunge na rais. Tumeweka pia masharti ya uteuzi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mbunge na diwani," alisema.

Dk. Mahera alisema kuwa kama mtu hajateuliwa, hajatekeleza masharti na kama mtu akitumia sababu nje ya hayo masharti hatafanikiwa.

"Huyo akikata rufani atashindwa. Tume inafanya kazi kuhakikisha kwamba shughuli zake zinafanyika kwa uwazi na uhuru na ukiangalia katika maelekezo ya wasimamizi wa uchaguzi, maelekezo kwa wasimamizi wa vituo vya kupiga kura, kwa vyama vya siasa na wagombea, yanaelekeza vizuri na yapo tovuti ya tume.

"Ukiona mtu anasema amekatwa, sijui hajateuliwa... maana yake ni vizuri uulize kwa msimamizi wa uchaguzi, akuelezee sababu ni nini, kwa mwenyewe ambaye hakupata uteuzi au upate ufafanuzi tume.

"Na sisi tume tupo tayari kushirikiana na ninyi ili uchaguzi huu uwe huru na haki, anayeshinda atangazwe, lakini tabia ya watu kuingia kwenye uchaguzi na hata kabla uchaguzi haujafanyika, tayari anajiona ni mshindi, hiyo ni tabia mbaya," alionya.

Dk. Mahera alisema sheria, kanuni na taratibu zitatumika kuhakikisha aliyeshinda ndiyo anapewa haki hiyo.

"Tunawasihi Watanzania msiingie kwenye vurugu zisizo na msingi na wale wagombea wote tumeanza leo (jana) Agosti 26, maadili ya uchaguzi 2020 kwa ajili ya rais, wabunge na madiwani yanaanza kutumika rasmi leo (jana). Kwa hiyo, sheria na adhabu zitakazoendana na hayo maadili zitaanza kutumika leo, hakuna uhuru huo tena," alisema.

Aliwataka wagombea kuzingatia vitabu vya maadili hayo na kuwakumbusha sheria nyingine za nchi hazijasimama katika kipindi hiki cha mchakato wa uchaguzi.

"Hayo matokeo (wagombea kupita bila kupingwa) hata mimi sijayapata, ni masuala ya mitandaoni jana (juzi) saa 10 jioni ndiyo tulianza kuweka majina, hao wote mnaosikia wanatangazwa bado hadi leo (jana) saa 10 jioni kama hakutakuwa na pingamizi ndiyo tume itapewa taarifa rasmi na wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya majimbo na hilo halijafanyika," alisema.

Dk. Mahera alisema kitendo cha kutangaza matokeo ni kinyume cha sheria kwa kuwa muda uliowekwa kwa ajili ya pingamizi bado haujaisha.

Alisema tume haitasita kuchukua hatua kwa chombo chochote cha habari kitakachoonekana kwenda kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.

## HABARI KITAIFA

# Maprofesa wakosoa wagombea vyama vya upinzani kuenguliwa

**Na Waandishi Wetu**

PROFESA Gaudence Mpangala wa Chuo Kikuu cha Katoliki Ruaha (RUCU), amekosoa kuenguliwa kwa wagombea wa vyama vya upinzani katika mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Amesema kinachotokea sasa kwenye mchakato huo kwa baadhi ya wagombea kuenguliwa kilianzia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa ambao ulilalamikiwa.

Msomi huyo alikuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mchakato wa uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Jumatano Oktoba 28, mwaka huu.

Alisema ili uchaguzi uwe huru na haki kama ambavyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imekuwa ikitangaza kila mara, ni lazima wahakikishe vyama vyote vinapewa haki ya wagombea wao kushiriki.

"Hii ni mbinu iliyotumika uchaguzi wa serikali za mitaa, wapinzani wakaenguliwa. NEC ilivyotangaza uchaguzi utakuwa huru na haki hatukutegemea hili lijirudie tena.

"Haiwezekani wagombea wanaoonekana fomu zao zina matatizo wawe wa upinzani tu. Mbona wa CCM hakuna anayerudishwa? Haiwezekani uchaguzi uwe huru na haki kama mfumo wenyewe hauruhusu uwe hivyo, hatuna tume huru," alionya.

Profesa Mpangala alisema kuwa, ili uchaguzi uwe huru na haki, wagombea wote wanatakiwa watendwe haki sawa, bila hivyo siyo wa haki.

Wakati Profesa Mpangala akisema hayo, Profesa Alexander Makulilo kutoka Idara ya Sayansi ya Utawala ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), aliiambia Nipashe jana kuwa siyo jambo la ajabu kwa chama tawala kupata wagombea wanaopita bila kupingwa kutokana na kuwa na faida ya kutekeleza ilani.

"Mimi kwangu sioni ajabu kuwapo na wagombea waliopita bila kupingwa. Hii siyo mara kwanza, uchaguzi wa vyama vingi ulianza tangu 1995, tukawa nao mwaka 2000, 2005, 2010, 2015, wagombea katika nyadhifa za ubunge, udiwani wamekuwa wakipita bila kupingwa.

"Faida ambayo chama tawala inapata ni kwamba kinakuwa kimetekeleza sera na ilani, chama cha upinzani kinakosa 'advantage' (faida) hiyo kwa sababu kinakuwa hakijatekeleza ilani, sababu hakikushinda uchaguzi," alisema.

Hata hivyo, msomi huyo alisema ni vigumu kwa mtu ambaye ni mpya kupita bila kupingwa ingawa wakati mwingine inatokea kama wananchi wamechoka na mbunge aliyekuwa madarakani.

"Mfano, rais akipita kwenye jimbo la mbunge wa upinzani akikuambia tunabadilisha matumizi ya fedha za fungu fulani, ujue ni serikali iliyopo madarakani," alisema.

Profesa Makulilo alisema ifahamike kuwa zipo sababu mbalimbali za mtu kupita bila kupingwa ambazo ni pamoja na kutotimiza masharti ya sheria ambazo ukishindwa kuzizingatia, mpinzani wako anatangazwa mshindi.

Alisema sheria zilizopo zimeweka fursa kwa watu kukata rufani na kuweka mapingamizi ili NEC kwa kutumia kanuni na sheria, mtu akileta ushahidi wake ukaonekana ni sahihi, basi uamuzi unatenguliwa.

Kuhusu malalamiko ya baadhi ya wagombea kuporwa fomu, Profesa Makulilo alisema kuwa kwenye uchaguzi, kuna mambo mengi na mnapokuwa mnashindana mtu anaweza akaamua kusema lolote.

Alishauri wenye malalamiko ya aina hiyo kuyapeleka kwenye vyombo husika ambavyo vitachuja na kutoa uamuzi na kama hawajaridhika na uamuzi wa NEC, kuna fursa ya kwenda mahakamani. "Watu wasizue taharuki, wafuate sheria, ukishindwa NEC unaona umeonewa, unakwenda mahakamani mpaka haki inapatikana," alisema.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Richard Mbunda, alisema alipata fursa ya kumsikiliza Msimamizi wa Uchaguzi Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro.

Alisema msimamizi huyo alieleza kuwa, kutokana na utaratibu waliopewa na NEC walijitahidi kuwapelekea wagombea walioteuliwa na vyama vyao watu wa kuwakagua ujazaji wa fomu kabla ya siku ya mwisho ambayo ni juzi.

"Hii ina maana katika mazingira kama haya, mtu hawezi kuja na fomu kwamba haijajazwa vizuri au kuwa na mapungufu. "Kama huu ndiyo utaratibu uliotolewa na NEC, basi ulikuwa ni mzuri na ungeepusha malalamiko ya watu kuiangalia NEC kama chombo kinachotumika na chama tawala, hii ni namna ambavyo NEC inatakiwa kujitathmini. "Lakini, wakati mwingine unaweza kukuta wasimamizi wa uchaguzi wanafanya mambo wakidhani kwamba wanakisaidia chama tawala kumbe wanakipaka matope na kuipaka matope serikali katika mchakato ambao ulitakiwa uwe huru na wa haki na CCM ingeshinda bila kelele zozote," alisema.

Dk. Mbunda alisema kuenguliwa kwa wagombea wa upinzani ni jambo linalofikirisha na NEC inatakiwa kujitathmini namna ambavyo inaendesha mambo yake.

Jana, NEC ilipiga marufuku vitendo vya baadhi ya wagombea kujitangaza kupita bila kupingwa, ikifafanua kuwa ni tabia mbaya kwa kuwa inachochea vurugu.

■**Imeandikwa na Romana Mallya na Thobias Mwanakatwe**



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede (kulia), akijadiliana jambo na Kamishna wa walipakodi wakubwa, Alfred Mregi (katikati) na Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayombo, baada ya kufungua semina ya walipakodi wakubwa kuhusu mfumo mpya wa uwakilishaji ritani za kodi kwa njia ya kielektroniki, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwinyi, Soud waahidi makubwa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAGOMBEA wawili wa urais wa Zanzibar jana walichukua Fomu Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa ajili ya kugombea nafasi hiyo kupitia vyama vyao.

Wagombea hao ni wa CCM, Dk Hussein Ali Mwinyi aliyefika ZEC saa 3:00 asubuhi na mgombea wa AAFP Said Soud aliyefika saa 5:00 asubuhi ambapo walikabidhiwa fomu hizo na Mwenyekiti wa ZEC, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud.

Akizungumza katika viwanja vya Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui baada ya kuchukua fomu hiyo, Dk Hussein Mwnyi, alisema endapo atapata ridhaa za Wazanzibari kuwa rais, atahakikisha anaimarisha uchumi na hatakuwa na aibu na wakwepa kodi.

Mwinyi alisema miongoni mwa vipaumbele vyake ambavyo vinatokana na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM mwaka 2020-2025, ni kuimarisha sekta ya viwanda na utalii kwa ajili ya kuzalisha ajira na uvuvi wa bahari kuu.

Alisema mikakati imewekwa katika kuwaandaa vijana kuingia katika soko la ajira kwa kuimarisha vyuo vya utalii na uvuvi ambavyo vitawaandaa vijana kuwa katika uvuvi wa bahari kuu.

Alieleza katika kuyafikiya malengo ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025, anakusudia kuzalisha zaidi ya ajira 300,000 ambazo zitawawezesha vijana kujiajiri na kuingia katika soko la ajira.

"Nataka niwape habari njema wapinzani wetu kwamba chama Cha Mapinduzi hakijagawanyika baada ya kumalizika kwa mchakato wa kura za maoni...tupo vizuri, wagombea wote walioshiriki mtawaona katika kipindi cha kampeni za uchaguzi," alisema.

Aidha, alisema amejipanga kufanya kampeni za kistaarabu za kushindana kwa hoja na sio matusi au kulumbana na kusababisha uhasama wa jaziba za kisiasa.

Alisema kampeni hizo zitafanywa kwa njia ya kisayansi kwa kujenga hoja, huku ilani ya uchaguzi ya CCM ikiwa ndiyo dira na muongozo wa kuwaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo na kubadilisha mustakabali wa maisha yao.

"Viongozi wenzangu katika kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu nawaomba tuhubiri amani na utulivu, kauli ambazo zitakuwa na lengo la kuwaunganisha wananchi na sio kuwagawa kwa kuwabagua,' 'alisema Dk. Mwinyi.

Aliwataka wanachama wa CCM kutobweteka na kujitokeza kwa wingi kwenda kupiga kura Oktoba 28, mwaka huu ili kukipa ushindi wa kishindo chama hicho.

**SOUD KUENDELEZA MAZURI YA DK. SHEIN**

Kwa upande wake, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu ZEC, mgombea urais wa Zanzibar kupitia AAFP, Soud alisema kuwa amechukua fomu hiyo ili kuiongoza Zanzibar.

Alisema endapo atapata ridhaa ya Wazanzibar ya kuwa Rais wa Zanzibar ataendeleza yale yote mazuri yaliofanywa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema katika kampeni zake atahakikisha anawafikia wananchi katika kuomba ridhaa yao na kufanya siasa za kistaarabu.

Mgombea huyo aliendelea na ahadi yake ya kuwanunulia bajaji waandishi wa habari kama atachaguliwa kwa sababu waandishi wa habari ni wapiganaji sawa na wanajeshi.

"Kila mwandishi wa habari Zanzibar ambae ana cheti cha uwandishi wa habari nitampatia bajaji mpya kutoka India," alisema Soud.


**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**COMMERCIAL CASE NO. 8 OF 2020**

**GA INSURANCE TANZANIA LIMITED ..........................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**GOLDSHIELD INSURANCE SERVICES (EA) LTD .............................DEFENDANT**

**DECREE:**

**WHEREFORE,** the Plaintiff prays for judgment and decree against the defendants as follows:
a. The sum of Tshs. 83, 592,938/= per paragraphs 3 and 4 hereof.
b. Interest on the said sum of Tshs. 83,592,938/= at the commercial rate from the date of default of payment to the date of judgment
c. Interest on the decretal amount at the court rate from the date of judgment till the date of payment in full.
d. Costs of this suit
e. Interest on the costs at the rate of 7% per annum the date of award thereof till full and final payment of the same
f. Further or other relief this Honorable Court may deem appropriate and fit and grant.

This matter is coming up for Default Jugdement on 19th day of August, 2020 before Hon. Dr. Deo John Nangela, Judge and delivered by Hon. H.S Mushi Deputy Registrar in the presence of Yusuph Sheikh, Advocate for plaintiff and in the absence of defendant.

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT;**

Default Judgment is hereby entered infavour of the plaintiff as follows:
1. The Defendant is ordered to pay to the plaintiff a sum of TZS 83,592,938/=
2. The defendant is hereby ordered to pay interest on the above sum at the commercial rate of 15% per annum, from the date of default of payment to the date of this Judgment until.
3. The defendant is hereby order to pay interest on the decretal amount at the Court rate of 7% from the date of judgment till the date of full payment.
4. The Defendant is condemned to pay the Plaintiff all costs pertaining to the prosecution of this suit.

Given under my hand and the seal of the Court this day of 19th day of August, 2020.

..........................................
**Dr. D. Nangela**
**JUDGE, HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**

**Extracted on 19th day of June, 2020**

# Uteuzi NEC wamkwamisha Lissu kortini

**Na Hellen Mwango**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, anayekabiliwa na kesi za uchochezi, jana alishindwa kufika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kutokana na mchakato wa kurudisha fomu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua muda mrefu.

Lissu ambaye ni mgombea urais wa CHADEMA katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, anakabiliwa na kesi mbili zilizokuwa zimepangwa kutajwa jana katika mahakama hiyo ya jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, alidai mahakamani kuwa kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC, Lissu na mgombea wake mwenza, Salum Mwalimu, walitakiwa kurudisha fomu za kugombea urais na kupatiwa za uteuzi juzi saa sita mchana kisha aanze safari za kurejea Dar es Salaam kuhudhuria kesi zake.

Hata hivyo, Wakili Kibatala alidai kuwa kwa bahati mbaya, hadi kufikia saa 2:30 usiku, wagombea hao walikuwa hawajatoka katika ofisi za tume hiyo jijini Dodoma, hivyo kusababisha ratiba zake za usafiri kurejea Dar es Salaam kuharibika.

"Mheshimiwa, kutokana na sababu hiyo, ninaiomba mahakama iridhie kuahirisha kesi hii na kupanga tarehe nyingine ambayo ninaamini mshtakiwa atakuwapo mahakamani," aliomba Wakili Kibatala.

Wakili wa Serikali Mkuu, Renatus Mkude, alidai kuwa kwa mazingira hayo yaliyoelezwa na wakili wa utetezi, hawana pingamizi, hivyo rai yao shauri hilo liahirishwe hadi tarehe nyingine.

Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kassian Matembele, aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 24 mwaka huu.

Katika kesi hiyo namba 123 ya mwaka 2017, Lissu anadaiwa kutoa maneno ya uchochezi wakati wa kampeni za uchaguzi mdogo wa Jimbo la Diman, Zanzibar Januari 11, 2017, akiwa eneo la Kibunju Maungani, Wilaya ya Magharibi B Mkoa wa Mjini Magharibi.

Inadaiwa kuwa siku hiyo, Lissu alisema: "Tangu mwaka 1964, Tanganyika ndiyo inayoamua nani atawale Zanzibar... Tangu mwaka 1964, Zanzibar inakaliwa kijeshi na Tanganyika, nani anayebisha?

"Tangu mwaka 1995, ikifika uchaguzi, askari wa Tanganyika wanahamia Zanzibar ili kuja kuhakikisha kuwa vibaraka wao wa Zanzibar hawaondoki na wananchi wa Zanzibar mnapigwa, mnateswa, mnauawa kwa sababu ya ukoloni wa Tanganyika kwa Zanzibar."

Pia, inadaiwa katika tarehe hiyo, Lissu alitamka kuwa: "Marehemu Karume alipoanza kushtuka mwaka 71, 72, akauawa, itakapofika tarehe 15 mwezi wa kwanza, mnaadhimisha miaka 53 ya kukaliwa kijeshi na Tanganyika.

"Jumbe aliondolewa Dodoma, na Ally Hassan Mwinyi alipewa urais wa Zanzibar Dodoma, na aliyempa ni Nyerere na si Wazanzibar... Marais wa Zanzibar wote ni 'made in Tanganyika'...

"Zanzibar wanatawaliwa na Tanganyika kwa kivuli cha Tanzania, Tanzania ni Tanganyika... Tanganyika ni kivuli tu cha kuikalia Zanzibar, cha kuigeuza Zanzibar koloni na makoloni huwa yanawanyanyasa yanaowanyonya kisiasa, kiuchumi na kuyakandamiza kijeshi...

"Mmetawaliwa na Tanganyika kisiasa miaka yote hii... Mohamed Shein hana lolote, ni kibaraka tu, siku watawala wakisema hatufai, ataondolewa tu kama alivyoondolewa Aboud Jumbe."



Mgombea udiwani Kata ya Kunduchi, Michael Urio (kulia), akirudisha fomu kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika kata hiyo, Deogratius Panga, kwa ajili ya kugombea nafasi hiyo, kabla ya kupewa ya uteuzi jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## CUF kuzindua kampeni za uchaguzi Septemba 3

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kinatarajia kuzindua kampeni zake Septemba 3, mkoani Mtwara.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF Taifa, Juma Kilaghai, wakati akizungumza na Nipashe.

"Tayari maandalizi kwa ajili ya uzinduzi yamekamilika na tunaamini kila kitu kitakwenda sawa kama kilivyopangwa," alisema Kilaghai.

Wakati CUF ikitangaza uzinduzi wa kampeni hizo, Chama Cha Mapinduzi (CCM), ndicho chama kilichokuwa cha kwanza kutangaza uzinduzi wa kampeni zake ambao unatarajiwa kufanyika Jumamosi wiki hii.

Akizungumzia kuhusu wabunge walioenguliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika kugombea ubunge kupitia chama hicho, Kilaghai alisema kufikia jana walikuwa wanafanya utaratibu wa kukata rufani kupinga uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo kadhaa waliofanya hivyo.

"Kuna wagombea wetu wameenguliwa katika baadhi ya maeneo kwa kuonewa, Kwa hiyo utaratibu wa kukata rufani unafanywa na tunatarajia kwamba kufikia jioni ya leo (jana), watakuwa wamekamilisha rufani zao," alisema Kilaghai.

"Watu wafahamu kwamba katika majimbo yale ambayo CCM imepita bila kupingwa kulikuwa na wagombea wa vyama vingine vya siasa... siyo kweli kwamba hakukuwa na wagombea, kwa hiyo lazima haki itafutwe na tumewaruhusu wagombea wetu wafanye hivyo," aliongeza.

Mgombea wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia CUF katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni Profesa Ibrahimu Lipumba wakati mgombea mwenza wake ni Hamida Abdallah.

Profesa Lipumba pia ndiye mwe-

# Korti ya Mafisadi yahukumu kina Kitilya kulipa mabilioni

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi, imewahukumu Kamishna wa zamani wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Harry Kitilya (70) na wenzake wanne kulipa fidia ya Sh. bilioni 1.5 kwa serikali baada ya kumwandikia barua ya kukiri makosa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Vilevile, mahakama hiyo imewataka kila mshtakiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja au kwenda jela miezi sita baada ya kukiri mashtaka ya kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani milioni sita.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Immaculata Banzi.

Mbali na Kitilya, washtakiwa wengine ni Maofisa wa Benki ya Stanbic, Shose Sinare (44), Sion Salomon (44), Kamishna wa Sera ya Uchunguzi wa Madeni wa Wizara ya Fedha na Mipango, Benason Shallanda (59), na msaidizi wake Alfred Misana (50).

Mapema mahakamani huko, DPP Biswalo Mganga, alidai mbele ya Jaji Banzi kuwa alipokea barua ya washtakiwa wakiomba kuingia makubaliano ya kukiri makosa yao na kwamba baada ya majadiliano, aliwafutia mashtaka 57 kati ya 58 yaliyokuwa yanawakabili.

Aliiomba mahakama hiyo ipokee makubaliano hayo na kuyasajili kwa mujibu wa sheria na upande wa utetezi haukuwa na pingamizi dhidi ya ombi hilo la DPP.

Jaji Banzi alisema mahakama imeyapokea makubaliano hayo kwa mujibu wa kifungu cha 194 (D) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019 ambayo inaelekeza kila mshtakiwa ahojiwe na mahakama ichukue majibu yake. Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, DPP Mganga alidai hawana rekodi ya makosa ya nyuma ya washtakiwa, hivyo aliomba kwa mujibu wa makubaliano, washtakiwa walipe Sh. bilioni 1.5 kama fidia ya hasara waliyosababisha.

Jopo la mawakili wa utetezi, likiongozwa na Wakili Alex Mgongolwa, lilidai washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza na kwamba mshtakiwa wa kwanza (Kitilya) ni mzee ambaye anakabiliwa na maradhi mbalimbali, hivyo afya yake siyo nzuri.

Pia, alidai washtakiwa wote wana familia wakiwamo wazazi wao ambao wanawategemea katika maisha yao na kitendo cha kukaa rumande kwa miaka minne na nusu, familia hizo zilikuwa kwenye mahangaiko ya kimya kimya.

"Kukiri kwao makosa kumeokoa rasilimali fedha na muda wa mahakama, lakini washtakiwa hawa wanatakiwa kulipa fidia. Katika mazingira hayo, unawaingiza katika madeni ili waweze kulipa fidia.

"Ni rai yetu katika utoaji wa adhabu, tunaomba uyazingatie utoe adhabu yenye unafuu na inayotekelezeka ili kukidhi haja ya sheria hii ambayo dhamira yake ni kupunguza mrundikano wa mahabusu," alidai Wakili Mgongolwa.

Jaji Banzi alisema amezingatia hoja za pande zote kwamba washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza na wamekiri makosa yao kwani kwa asili ya kesi hiyo, ingechukua muda mrefu.

"Pia, kwa kuzingatia makubaliano waliyofikia, mahakama inawahukumu kulipa faini ya Sh. milioni moja au kifungo cha miezi sita jela kila mmoja. Washtakiwa wote mlipe fidia ya Sh. bilioni 1.5 kwa serikali ya Tanzania kwa hasara iliyopatikana," alifafanua Jaji Banzi.

Awali, akisoma mashtaka mapya, Wakili wa Serikali Mkuu, Oswald Tibabyekomya, alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kusababisha serikali hasara.

Alidai kuwa Mei Mosi 2012 na Juni Mosi 2015, wakiwa jijini Dar es Salaam, isivyo halali, washtakiwa waliandaa ada ya mkopo kwa Serikali ya Tanzania wa Dola za Marekani milioni 600,000,000 kutoka asilimia 1.4 hadi 2.4 na kusababisha serikali kupata hasara ya Dola za Marekani milioni 6,000,000.

# TCU yafungua dirisha maombi vyuo vikuu

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu (TCU), imefungua dirisha la maombi ya udahili wa shahada ya kwanza kwa mwaka wa masomo 2020/21 na kuwatahadharisha waombaji kuepuka kupotoshwa na mawakala.

Katibu Mtendaji wa TCU, Profesa Charles Kihampa, alitangaza kufunguliwa kwa dirisha hilo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana.

Alisema dirisha la kwanza la maombi ya udahili wa shahada ya kwanza limefunguliwa na litakuwa wazi hadi Septemba 25 mwaka huu.

"TCU inawaasa wananchi kuepuka kupotoshwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya namna ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu," alisema.

Aliwataka wanaohitaji kupata ufafanuzi wa suala lolote linalohusu udahili, wawasiliane na vyuo husika moja kwa moja au TCU kwa maelezo ya jumla kwa kutumia mtandao wao. Alisema waombaji wenye vyeti vilivyotolewa nje ya nchi, ni lazima wawasilishe Baraza la Mitihani (NECTA) au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), ili kupata ithibati ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kuanza kuomba udahili.

Profesa Kihampa pia aliwahimiza waombaji kuendelea kupata taarifa rasmi kupitia tovuti ya TCU na kubainisha kuwa udahili huo utahusisha makundi ya waombaji.

Aliyataja makundi hayo kuwa ni wenye sifa stahiki za kidato cha sita, wenye sifa za stashahada au linganifu na wenye sifa stahiki za programu ya awali ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Katika hatua nyingine, Profesa Kihampa alisema TCU imeandaa maonyesho ya 15 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yatakayofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja kuanzia Agosti 31 hadi Septemba 5 mwaka huu na kuwahimiza waombaji wa udahili kuhudhuria.



Vijana wakiandaa kitoweo cha pweza kwenye mazingira ya wazi bila ya kuchukua tahadhari ya vumbi, kitendo kinachoweza kuhatarisha afya za walaji, katika viwanja vya Mwijuma Mwananyamala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kikao kujadili bajeti EAC chakwama

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

KIKAO cha Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) cha kujadili bajeti ya bunge hilo kimekwama baada ya wabunge kutoka Kenya kususia kwa sababu ambazo Spika wa Bunge, Martin Ngoga, amesema hazijajulikana.

Akizungumzia baada ya kikao hicho kilichokuwa kinafanyika kwa njia ya mtandao kukwama, Ngoga alisema amelazimika kukiahirisha kwa mujibu wa kanuni za bunge na kwamba kitafanyika siku nyingine.

Ngoga alisema ataendelea kufuailia kujua sababu za wabunge hao kushindwa kuhudhuria kikao hicho ambacho alisema kina umuhimu mkubwa hasa wakati huu ambao Jumuiya inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uhaba wa fedha unaochangiwa na baadhi ya nchi kuchelewesha michango.

Naibu Katibu Mkuu wa Jumiya hiyo anayeshughulikia miundombinu, Mhandisi Steven Mlote, alisema taarifa alizo nazo ni kwamba ya wabunge wa Kenya kutoonekana ni matokeo ya mgomo baridi unaofukuta kati ya wabunge wa jumuiya hiyo na sekretarieti.

Alisema mgomo huo unatokana na hatua ya wabunge hao kutaka walipwe mamilioni ya fedha ambazo haziko kwenye utaratibu wa kisheria katika jumuiya.

Kwa mujibu wa Mlote, wabunge hao wanashinikiza kulipwa dola 560 kwa ajili ya posho za vikao, safari na malazi jambo ambalo haliwezekani kutokana na vikao vingi kufanyika kwa njia ya mtandao. Alifafania kwamba fedha halalli wanazotakiwa kulilpwa ni dola 160 ambazo wameshalipwa lakini wanashinikiza kulipwa tena dola 400 za safari ambazo hazikufanyika.

Mlote alisema kimsingi utekelezaji wa matakwa ya wabunge hao ni mgumu kwa kuwa hadi sasa wanataka kulipwa zaidi ya dola milioni mbili za kimarekani ambazo licha ya kwamba hazipo, utaratibu huo ni kinyume cha sheria za jumuiya

Akizungumzia suala hilo kwa njia ya simu, mmoja wa wabunge wa bunge hilo kutoka Tanzania, Dk. Makame Abdulla, alikanusha kuwapo kwa mpango wa wabunge wa kugomea kikao kwa sababu za shinikizo la kulipwa madeni na kufafanua kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu na linawakabili wafanyakazi wengi wa jumuiya hiyo.

Kuhusu hatua iliyofikiwa ya michango, Mlote alisema hadi sasa Burudi na Sudani Kusini bado hazijakamilisha michango yao na kwamba zingine zote zimeshalipa.



## ARUSHA TECHNICAL COLLEGE

### Specific Procurement Notice
### REQUEST FOR BIDS Goods
### (One-Envelope Bidding Process)

| | | |
|---|---|---|
| **Country** | : | **TANZANIA** |
| **Name of Project** | : | **EAST AFRICA FOR TRANSFORMATION AND REGIONAL INTEGRATION PROJECT (EASTRIP)** |
| **Contract Title** | : | **SUPPLY OF ONE MOTOR VEHICLE AND TWO MOTORCYCLES FOR KIKULETWA RENEWABLE ENERGY TRAINING AND RESEARCH CENTRE** |
| **Loan No** | : | **63330** |
| **RFB Reference No.** | : | **TZ-ATC-189830-GO-RFB** |

1. The Arusha Technical College through the Government of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of East Africa for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP) and intends to apply part of the proceeds toward payments under the contract for Supply of One Motor Vehicle and Two Motorcycle for Kikuletwa Renewable Energy Training and Research Centre for this contract, the Borrower shall process the payments using the Direct Payment disbursement method, as defined in the World Bank's Disbursement Guidelines for Investment Project Financing, except for those payments, which the contract provides to be made through a letter of credit.

2. The Arusha Technical College through Kikuletwa Renewable Energy Training and Research Centre now invites sealed bids from eligible Bidders within the delivery period of 120 days for Supply as described in the following table:-

| S/N | Bid Description | Lot No. |
|---|---|---|
| 02 | Mini bus, Fifty to Fifty five 50 - 55 passengers seats | 02 |
| 03 | Supply of two Motorcycles | 03 |

The bidder can be eligible to bid for one lot, two lots or all three lots.

3. Bidding will be conducted through National Competitive Procurement using a Request for Bids (RFB) as specified in the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers"1st July 2016 and revised November 2017 ("Procurement Regulations") and is open to all eligible Bidders as defined in the Procurement Regulations.

4. Interested eligible Bidders may obtain further information from the Arusha Technical College, Att: Tender board Secretary, email: **pmu@atc.ac.tz** inspect the bidding document during office hours from 0800 to 1600 Monday to Friday inclusive except on public holidays at the address given below.

5. The bidding document written in English Language may be issued to the interested Bidders upon the submission of a written application to RECTOR, ARUSHA TECHNICAL COLLEGE, P. O. Box 296, Moshi- Nairobi Road, Arusha, Tanzania email address: **rector@atc.ac.tz** or **Phone no. +255 27 29 70 056**

6. Bids must submit one original and two copies of the documents, properly filled in, enclosed in plain sealed envelopes and must be delivered to the RECTOR, ARUSHA TECHNICAL COLLEGE, ATTENTION: Tender board Secretary, Office: Administration Building Room No.104, First floor, Arusha, Tanzania at or before 11.00 am on 15th September, 2020. Electronic Bidding will not be permitted. Late Bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the Bidders' designated representatives and anyone who chooses to attend at the Arusha Technical College-Board Room, Room No.105 at 11.00am on 15th September, 2020.

7. All Bids must be accompanied by a Bid Security Declaration in the Format provided in the form of Request for Bids (RFB).

8. "Attention is drawn to the Procurement Regulations requiring the Borrower to disclose information on the successful bidder's beneficial ownership, as part of the Contract Award Notice, using the Beneficial Ownership Disclosure Form as included in the bidding document."

**RECTOR**
**ARUSHA TECHNICAL COLLEGE**
**P. O. Box 296, Arusha**
**E-mail: rector@atc.ac.tz**
**Website: www.atc.ac.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# LATRA, TABOA wakubaliane ukatishaji tiketi kimtandao

**MWISHONI** mwa wiki Umoja wa Wamikili wa Mabasi Tanzania (TABOA), ulitoa malalamiko juu ya uwapo wa tozo nyingi kwenye kukata tiketi kwa mtandao, kwa maelezo kuwa ni kiongeza gharama za uendeshaji.

Kikao hicho kilijumuisha maofisa kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa lengo la kujadili kanuni mpya za sheria ya usafirishaji zilizoleta utaratibu wa kukatisha tiketi kielektroniki.

Kwa mujibu wa kanuni hizo zinazolalamikiwa, ni LATRA kupata asilimia 0.5 ya fedha iliyokatwa kwenye tiketi, huku wasafirishaji wakihoji kwanini fedha hizo zinatozwa kwenye pato ghafi.

TABOA ilidai kutupiliwa mbali kwa maoni yao juu ya kanuni hizo ambayo pamoja na mambo mengine walipendekeza kutumika kwa mashine za EFD.

TABOA pia inalalamikia tozo ya asilimia mbili kwa mzabuni atakayeendesha mfumo, huku wakieleza walipata mzabuni ambaye alikubali kutoza asilimia 0.7, lakini LATRA ilimpitisha iliyemtafuta.

Kwa ujumla, kilio cha wasafirishaji ni kuongezeka kwa tozo ambazo moja kwa moja zinakwenda kuongeza gharama za uendeshaji na pendekezo wanalokuja nalo ni LATRA kama inataka kukusanya fedha hizo kutoka kwa wasafirishaji iongeze ngarama za nauli.

Kadhalika, kilio kikubwa ni tozo ya asilimia 0.5 inayochukuliwa na LATRA kwa mtoa huduma wakati yeye ni msimamizi ambaye hulipwa mshahara kutoka hazina.

Kwa ujumla kilio hiki kinatoa taswira kuwa wadau hawa (LATRA na TABOA) hawataki kukubaliana na hakukuwa na mazungumzo yaliyowafikisha kwenye kukubalinana na kutokukubaliana au upande mmoja ukikubali kupoteza sehemu ya yale wanayoamini, hivyo ni muhimu kwa pande zote kukubaliana (win win situation).

Upo usemi usemao kuwa tembo wakipigana zinazoumia ni nyasi, hii ni kutokana na ukweli kuwa wanaokizana ni wakubwa wawili, mmoja ameshika mpini na mwingine makali, lakini wote wanategemeana kwa kuwa hakuna LATRA kama hakuna wasafirishaji, na lazima awepo kwa ajili ya kusimamia usafiri wa ardhini nchini.

Ni lazima kuwe na meza ya makubaliano kwa kuwa tunaona yapo mambo ya msingi ambayo TABOA wanahoji, kama kutumika kwa mzabuni wa bei nafuu ambaye hataumiza wasafirishaji.

Lakini ipo hoja ya kwanini LATRA kama msimamizi anajiongeza jukumu la kukusanya fedha kutoka kwa anaowasimamia, badala ya kubaki na jukumu la msingi la usimamizi.

Tunaona jambo hili halipaswi kubaki lilivyo kwa kuwa litawafanya wanaosimamia kuona wanaonewa, na anayesimamia kuona ana haki ya kufanya hivyo kwa kuwa tu ameshika kwenye mpini.

Ni muhimu sana kama ilivyokuwa awali kuwa na mazungumzo ya kuwezesha pande zote kuelewana kuliko kutumia nguvu na mamlaka, jambo ambalo linaweza likaathiri utekelezaji na mwisho, hivyo kuwaumiza walaji. Kilio cha wadau wa LATRA kisikilizwe, na wakati huo maslahi ya mlaji yalindwe ili kuepuka gharama za uendeshaji zitakazoongezeka kubebwa na mlaji. Mvutano huu hauna afya sana kwa pande zote zinazotegemeana, kwa kuwa TABOA wana hoja za msingi za kueleza kwanini wanafikiri LATRA hastahili kukusanya asilimia 0.5 ya pato ghafi wanalopata wasafirishaji.


Jingine, wanaona ni vyema kazi ya kukusanya kodi ikaachwa mikononi mwa TRA, na zitumike mashine ya EFD ambazo hazina gharama, kuliko kutumia mashine za POS ambazo msafirishaji atatakiwa kuweka fedha kwanza.

Kilio cha wasafirishaji kinachofanana na hicho ni cha madereva wa teksi au magari mtandaoni ambao wanatakiwa kulipa Sh. 35,000 kwa ajili ya kupata leseni, wakati huo bado hakuna usimamizi sahihi wa kuhakikisha tozo zinazotozwa na mmiliki wa mtandao zina uhalisia.

Tunatarajia wahusika wataketi pamoja na kupata muafaka wa kudumu, ambao unauwezesha kila upande kutekeleza vyema majukumu yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Wapigakura fursa kuhoji iwapo afya ni kipaumbele cha vyama

Na Sabato Kasika

**PAZIA** la kampeni za uchaguzi mkuu, liliachwa wazi kuanzia jana, ili wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi wajinadi kwa wananchi na hatimaye Oktoba 28, yafanyike maamuzi wawachague au wawaache.

Kuchaguliwa ama kuachwa kwa wagombea, kutategemea ni jinsia gani wapigakura watakavyokuwa wameridhika au kutoridhika na ilani za vyama ambazo zitanadiwa katika kampeni hizo.

Jambo mojawapo la msingi la kuzingatia ni kwamba, ujenzi wa uchumi imara wa familia na hata taifa hutegemea wananchi wenye afya njema na wenye uhakika na matibabu, kwa kuwa afya ni mtaji wa maisha.

Afya inaelezwa kuwa ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili, kijamii na kutokuwapo kwa maradhi. Ndiyo nguzo na rasilimali muhimu katika kuchangia maendeleo ya mtu binafsi, familia na nchi hususan katika kuleta maisha bora na kupunguza umaskini.

Kwa mantiki hiyo, afya inalenga kuwa na ustawi endelevu kwa jamii, kwa kuzingatia mchango wa mtu binafsi kulingana na nafasi, uwezo na fursa zilizopo katika kuleta maisha bora.

Vilevile upatikanaji wa afya bora unahitaji uwezeshaji wa jamii iwe na uwezo wa kushiriki, kuamua, kupanga na kutekeleza mikakati yao ya kuwaletea maendeleo katika ngazi mbalimbali.

Hivyo, ujenzi wa miundombinu ya afya ni muhimu uendane na huduma husika, kutokana na umuhimu huo, ikiwamo mgawanyo wa wataalamu na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba maeneo yote nchini ili wananchi wahudumiwe kikamilifu.

Lakini, Tanzania ina sera ya taifa inayotaka wazee wasiojiweza kupatiwa matibabu bure, ambayo utekelezaji wake unaendelea ikiwamo kuwagawia vitambulisho kwa ajili ya kupata huduma hiyo bure.

Sera hiyo imefungua milango kwa wazee wasiojiweza kupatiwa matibabu bure, hivyo ni vyema kasi ya kutoa vitambulisho ikaendelezwa zaidi na kama ilani zitakuwa zimeiwekea msukumo.

Ndiyo maana hoja hii inalenga kila chama kilichoandaa ilani ya uchaguzi itakayowasilishwa kwenye kampeni za mwaka huu iainishe kazi za wagombea hadi 2025, iwe imeeleza mambo mbalimbali ambayo kinatarajia kuyafanya kitakapopewa ridhaa ikiwamo kuboresha afya.

Ikumbukwe kuwa msingi mkubwa wa kuweza kuleta unategemea afya bora ya wananchi, hivyo ilani za vyama ziweke wazi jinsi ambavyo vitaboresha afya za Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Kwa mfano, ilani ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2020, ilitangaza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ili kufanikisha kuimarisha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Matarajio yalikuwa ni kila kijiji kuwa na zahanati, kata kuwa na kituo cha afya na wilaya kuwa na hospitali, kwa ajili ya kuleta mabadiliko, ambayo ni kuwa wananchi wenye afya bora watakaoweza kushiriki, katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kutoa huduma katika mitano ijayo.

Katika utekelezaji wa ilani hiyo ya CCM kwa upande wa afya, imefanya juhudi za kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali, kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Juhudi hizo zinatakiwa kuongezwa, ili kuhakikisha vijiji vyote, kata na wilaya zinakuwa na huduma hiyo muhimu yenye lengo la kuboresha afya za Watanzania, waweze kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Hata Sera ya Afya ya mwaka 2007, inatambua hilo, huku ikiwa na dira, ambayo ni kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi inayochangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi.

Mbali na dira, sera hiyo pia ina makusudio, ambayo ni kutoa huduma muhimu za afya zenye uwiano wa kijiografia, viwango vya ubora unaokubalika, gharama nafuu na zilizo endelevu.

Upande wa madhumini ya sera hiyo, ni kuinua hali ya afya ya wananchi wote, hasa wale walioko katika hatari zaidi, kwa kuweka mfumo wa huduma za afya utakaokidhi mahitaji ya wananchi na kuongeza umri wa kuishi wa Watanzania.

Njia mojawapo za kuongeza umri wa kuishi zinatajwa katika sera kuwa ni huduma bora za afya, kwa kuzingatia mahitaji ya makundi maalum yakiwamo watoto wachanga, wajawazito na wazee.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi wajisaidia porini kwa kukosa vyoo

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

ZAIDI ya wanafunzi 1,000 katika Shule ya Msingi Sirari, Tarime mkoani Mara, wanalazimika kujisaidia katika maeneo hatarishi ikiwamo porini kutokana na ukosefu wa matundu ya vyoo.

Wazazi wa wanafunzi na wakazi wa Kata ya Sirari waliazimia katika mkutano mkuu wa mwaka ulioketi wiki hii shuleni hapo kuchangia kwa hiari kiasi cha Sh. 1,000 kila mmojai ili kunusuru changamoto hiyo, huku waalimu wakiwaomba wadau wa maendeleo kuchangia haraka.

Mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo, Samuel Togo, alisema baadhi ya wazazi walitafsiri vibaya uamuzi wa serikali kutoa elimu bila malipo, na kushindwa kutekeleza wajibu wa kushiriki katika shughuli za maendeleo, ukiwamo ujenzi wa miundombinu shuleni.

"Tunawakumbusha wazazi kwamba ingawa serikali ilitangaza kuondoa ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne, lazima washiriki kikamilifu katika ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa kuchangia kwa hiari bila kutegemea serikali kufanya kila kitu," alisema.

Alisema mbali na uchakavu wa miundombinu ya vyoo, shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa vinne kwa ajili ya kuhimili ongezeko la wanafunzi waliosajiliwa darasa la kwanza mwaka 2020, ambao darasa moja linatumiwa na wanafunzi zaidi ya 60.

Katika hatua nyingine, Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Kennedy Muniko, alisema kutokana na likizo ya Corona, wanafunzi zaidi ya 84 hawajaripoti shuleni, na kwamba hakuna taarifa zozote kuhusu walipo, hivyo kuwataka viongozi wa vijiji kuhakikisha wanawasaka watoro hao.

Alisema wazazi waliokatisha masomo na walioozesha watoto wao wa kike na wanaowatumikisha katika shughuli za kiuchumi, watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa kortini.




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa Barabara ya Mwakangale katika Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. Barabara hiyo, ilikuwa kero kubwa kwa wananchi wa eneo hilo, hasa kipindi cha mvua. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC atoa dawa kumaliza migogoro ardhi

**Na Julieth Mkireri,** MAFIA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesema elimu kwa wajumbe wa mabaraza ya ardhi ndilo suluhisho la kumaliza migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Amesema iwapo wenyeviti wa mabaraza ya ardhi ya wilaya watatoa semina kwa wajumbe wa mabaraza hayo ngazi ya kata, idadi ya wananchi wanaokimbilia kwenye mabaraza ya wilaya kutafuta haki zao itapungua.

Ndikilo alitoa wito huo juzi mjini hapa baada ya kuwaapisha wajumbe wa Baraza la Ardhi la Wilaya hiyo.

Alisema wajumbe hao wanatakiwa kupatiwa semina kutokana na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaoshindwa kupata haki zao na badala yake kukimbilia ngazi ya wilaya kutafuta haki. Aidha, Ndikilo aliwataka wanasheria ngazi ya halmashauri kuhakikisha wanawasaidia wananchi kukata rufani hata nje ya muda uliowekwa ili kupata haki zao.

"Baadhi ya wananchi wanashindwa kupata haki zao kwa kucheleweshewa nakala ya hukumu lakini wengine wanakwama kukata rufaa (rufani) kwa muda unaotakiwa. Kutokana na vikwazo hivyo, wanasheria kwenye halmashauri wanatakiwa kuwasaidia wananchi hawa wanyonge," alisema.

Aliwataka wajumbe wa mabaraza ya ardhi kusikiliza mashauri bila kuchoka, lakini kutoa hukumu kwa haki na nakala zitoke kwa wakati.

"Wananchi wengi ni wanyonge kimbilio lako kubwa ni kwenye haya mabaraza ya ardhi kupata haki zao. Kataeni rushwa, tendeni haki wakati mnaendesha kesi ili kumaliza hii migogoro ya mara kwa mara katika haya mabaraza," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya za Mafia, Mkuranga na Kibiti, Rehema Mwakibuya, aliahidi kushughulikia maagizo ya mkuu huyo wa mkoa.

Awali, wananchi wa Mafia walikuwa wakisafiri hadi Mkuranga kusikiliza kesi zao za ardhi jambo ambalo ilikuwa kikwazo kwao kutokana na baadhi yao kushindwa kumudu gharama za ndege na usafiri wa majini.

Mkoa huo una mabaraza 128 ya ardhi ya kata ambayo yamekuwa yakishughulikia migogoro ya ardhi ambayo mingi inaelezwa kusababishwa na uwapo wa mashamba yasiyoendelezwa.

# Waonywa kutumia vyandarua kilimo

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WANANCHI waonywa kutumia vyandarua vinayotolewa na serikali kwa lengo la kupunguza kasi ya ugonjwa wa malaria kwa shughuli za uvuvi na kilimo cha bustani.

Angalizo hilo lilitolewa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Afya Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Rashid Maftah, jana wakati akizungumza na wanahabari kuhusiana na kampeni ya kutokomeza ugonjwa wa malaria unaoambatana na ugawaji wa vyandarua vya bure kwa wananchi.

Alisema serikali imeendelea na kampeni hiyo yenye lengo la kutokomeza ugonjwa huo nchini, na kwamba hadi sasa vyandarua milioni 47 vimeshatolewa bure katika mikoa mbalimbali nchini kuwezesha wananchi kujikinga na mbu kama njia ya kutokomeza kabisa malaria .

"Tumeendelea kugawa vyandarua hivi ili kuikinga jamii na ugonjwa huu hatari wa malaria ila nitoe wito kwa jamii kutumia vyandarua hivi kwa malengo yaliyokusudiwa badala ya kuvigeuza kuwa nyavu za kuvulia samaki ama uzio wa kuzuia kuku na ndege kuharibu bustani zao za mboga... haya si malengo ya serikali kusambaza vyandarua hivi," alisema.

Alisema awali kulikuwa na malalamiko mengi kuhusiana na vyandarua hivyo vinavyotolewa kuwa ni vidogo havitoshi katika vitanda vya baadhi ya wananchi, lakini kwa sasa malalamiko hayo yamefanyiwa kazi na kuleta vyandarua ambavyo ni vikubwa zaidi vinavyotosha vitanda vya aina zote.

Alisema wameshasambaza vyandarua kwa zaidi ya asilimia 100 nchini, jambo ambalo ni la kujivunia na kuipongeza serikali kwa kuliwekea mkazo zaidi suala la afya ya Watanzania kwa kuamua kugawa bure vyandarua nchini .

Kuwa kampeni hiyo ya ugawaji wa vyandarua imehusisha awamu tatu, ambapo awamu ya kwanza ilihusisha mikoa ya Rukwa, Mbeya na Songwe na awamu ya pili hii itahusisha Iringa, Singida na Dodoma.

Aliwataka wananchi kujitokeza kujiandikisha ili kunufaika na mpango huo wa serikali wa ugawaji wa vyandarua bure.

Naibu Meneja wa Mpango wa Kudhibiti Malaria nchini, Dk. Samuel Nhiga, alisema kuwa ukilinganisha na miaka mitano iliyopita kwa sasa kiwango cha malaria nchini kimeendelea kupungua kwa kasi.

Aliitaja mikoa ambayo ina kiwango cha chini cha malaria nchini nii Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Iringa na Njombe.



Mkurugenzi wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel (kushoto), akizungumza na vijana waliomaliza vyuo vikuu nje ya nchi kuhusu namna wanavyoweza kujiajiri na kutafuta ajira mafunzo yaliyoendeshwa na Sekretarieti ya Ajira jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Viongozi na wagombea watakiwa kudhibiti wafuasi kwenye kampeni

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

VIONGOZI wa vyama vya siasa katika Jimbo la Bukoba Mjini, wametakiwa kuwadhibiti wafuasi wao na kuhakikisha hawawi chanzo cha vurugu na kuhatarisha amani iliyopo.

Msimamizi wa Uchaguzi katika Jimbo la Bukoba Mjini ambaye ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, Limbe Morris, alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumzia urejeshaji fomu za wagombe ubunge na kuanza kwa kampeni.

Morris alisisitiza kuwa chama chochote kitakachofanya kampeni za vurugu kitachukuliwa hatua. "Kila kiongozi atakayekuwa akishiriki kwenye kampeni lazima atumie lugha ya staha ambayo itawawezesha wananchi kutambua sera za chama husika. Sitarajii chama chochote kwenda katika mkutano kuuza matusi badala ya sera. Wauze sera na waeleze watawafanyia nini wananchi wakiwachagua," alisema.

Akizungumza baada ya kurejesha fomu mgombea ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika jimbo hilo, Steven Byabato, aliahidi kutumia ilani ya chama chake kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

"Katika Jimbo la Bukoba Mjini zipo changamoto ndogo ndogo tu zinazowakabili wananchi ambazo haziko katika ilani ya CCM.

Kwa kuwa mambo mengi na makubwa yapo katika ilani yetu ya mwaka 2020 hadi 2025, basi tutakaa na chama na wananchi na kuelekezana vizuri na baadaye changamoto hizo zitapatiwa ufumbuzi," alisema.

Mgombe ubunge kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chief Kalumuna, aliwataka wana-CHADEMA kushirikiana kuomba kura kwa wananchi, na kuzilinda siku ya kupiga kura. "Tushirikiane kuzitafuta, lakini tushirikiane kuzilinda ili aliyeshinda ndiye atangazwe kuliongoza jimbo hili," alisema Kalumuna. Wagombea sita wa kiti hicho kutoka CCM, CUF, CHADEMA, NLD, NCCR- Mageuzi na ACT Wazalendo waliochukua fomu, wote wamerejesha na kukidhi vigezo vya kugombea ubunge katika Jimbo la Bukoba Mjini.

# Wateja wa Vodacom wapewa huduma mpya

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania, imezindua huduma nyingine ijulikanayo kama Jimixie bando inayowapa wateja uhuru na urahisi wa kujitengenezea mseto wa bando zao wenyewe kutegemeana na mahitaji yao, muda wa kuisha kwa bando, motisha na gharama.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara wa Vodacom, Linda Riwa, alibainisha hayo wakati alipozungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo mpya, na kusema kwa miaka mingi kampuni hiyo imeonyesha mfano katika uvumbuzi na kujenga jamii ya kidijitali kwa kuzindua huduma za pekee na za kwanza sokoni. "Kwa kutambua kwamba mahitaji ya kila mteja ni tofauti na wakati huo huo wateja wote wanahitaji kupata thamani zaidi kwa kile wanachokilipia, tumeamua kutengeneza huduma ambayo inawapa uhuru wa kupata kile wanachohitaji na kwa gharama ambayo wako tayari kuilipa.

"Mteja anaweza akatengeneza bando lake mwenyewe lenye Data, SMS na Dakika za maongezi kwa pamoja kutegemeana na mahitaji yake, kwa gharama anayoimudu na kwa muda wa kuisha kwa bando wanaoutaka. Huu ni ushahidi wa namna ambavyo tunawajali wateja wetu kwa kuwapatia uhuru wa kutengeneza mseto wa bando yao wenyewe," alisema Riwa.

"Kwa mara ya kwanza nchini, wateja watakuwa na uwezo wa kuchagua ni kiasi gani wanataka kutumia, na wanataka kutumia katika huduma gani. Tutaendelea kuzindua huduma zenye ubunifu kwa wateja wetu ili kuhakikisha kwamba wanapata huduma za kipekee kwenye mtandao bora na wa kisasa popote pale walipo wakiwa na Vodacom," alisema Riwa.

Naye Mkuu wa Idara ya Mikakati na Huduma kwa Wateja, Jackson Walwa, alisema huduma hiyo inapatikana kwa wateja wote na katika mifumo yote ya simu za kawaida na simujanja. Mteja atakuwa na uwezo wa kutengeneza bando lake mwenyewe kutegemeana na anataka nini na huduma anayoweza kuimudu.

# RAS akerwa na watumishi kukaa ofisini

**Na Julieth Mkireri,** MAFIA

KATIBU Tawala Mkoa wa Pwani, Dk. Delphine Magere, amewataka watumishi kuacha tabia ya kukaa ofisini na badala yake wajenge tabia ya kuwafikia wananchi na kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka.

Dk. Magere alitoa wito huo juzi wilayani hapa alipokuwa akizungumzia na wakazi wa kata ya Kirongwe wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo.

Ndikilo alifanya ziara hiyo kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi katika halmashauri zote za mkoa wa Pwani.

Alisema huu si wakati wa kukaa na matatizo ya wananchi na kila mmoja anatakiwa kuwajibika ipasavyo kutekeleza wajibu wake bila kusubiri msukumo kutoka ngazi za juu.

"Zama zimebadilika tuache kukaa ofisini. Tutoke tukawasikilize wananchi tunaowawajibikia wakati mwingine wanaotukwamisha ni watumishi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati," alisema.

Katibu tawala alisema iwapo kila mmoja atasimamia majukumu yake ipasavyo, atasaidia kupunguza kero za wananchi ambazo hazitafutiwi ufumbuzi kwa wakati na kuwafanya wananchi kufanya shughuli za maendeleo na kujikwamua na hali ya maskini kwenye maeneo yao.

"Tusikae na matatizo ya wananchi, tujenge tabia ya kuwasikiliza. Watumishi kuanzia ngazi za chini, tukifanya hivyo hata viongozi wa juu hawapati shida wanapotembelea maeneo hayo," alisisitiza.

Akiwa Mafia, Ndikilo aliahidi kuwa serikali ya mkoa kwa kushirikiana na wilaya, watasimamia miradi ya maendeleo ambayo haijakamilika kutekelezwa kwa wakati na kuwasaidia wananchi wa maeneo husika.

HABARI KITAIFA




Mkuu wa Kitengo cha Mikakati na Thamani kwa Wateja wa Vodacom Tanzania Plc, Jackson Walwa, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu bando jipya la Vodacom Jimixie linalowapa wateja uhuru na urahisi wa kujitengenezea mseto wa bando zao wenyewe kulingana na mahitaji yao. Kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara wa kampuni hiyo, Linda Riwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEMC kuwaburuza kortini wachafuzi wa kelele, mitetemo

**Na Mwandishi Wetu**

KUFUATIA kuwapo kwa wimbi kubwa la uchafuzi wa kelele na mitetemo jijini Dar es Salaam na mikoa ya jirani, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeonya litawafikisha mahakamani wahusika wote kama hatua ya kudhibiti hali hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema jijini Dar es Salaam kuwa baraza halitomwonea mtu bali hatua zitachukuliwa kukidhi matakwa ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na kanuni ya uchafuzi wa kelele na mitetemo ya mwaka 2015.

"Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni yake inayosimimia uchafuzi wa kelele na mitetemo ya mwaka 2015 imeweka wazi viwango vya sauti katika viwanda, maeneo ya biashara pamoja na maeneo ya taasisi za elimu. NEMC tutaitumia sheria hiyo kuhakikisha changamoto hiyo inaondoka na kuwapa utulivu wa kutosha wananchi," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema NEMC imechukua hatua kadhaa kuhakikisha wenye baa, kumbi na nyumba za starehe wanadhibiti uchafuzi wa kelele na mitetemo, lakini wimbi la uchafuzi huo limeongezeka na ushahidi ni kuongezeka kwa malalamiko ya wananchi.

"Tumekuwa tukipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusiana na kelele zinazotoka katika kumbi za starehe, mabaa na baadhi ya nyumba za ibada. NEMC tumechukua hatua kadhaa ikiwamo kutoa elimu, kuwaonya baadhi ya wahusika na utozaji faini lakini malalamiko yameongezeka na tumejipanga kuchukua hatua za juu zaidi na kuwafikisha mahakamani," alisema.

Dk. Gwamaka alisema kelele hizo zimekuwa kero kwa wakazi wa maeneo husika hususani kushindwa kusoma kwa utulivu, kuwaathiri wagonjwa pamoja na wananchi kushindwa kupata mapumziko mazuri, hasa nyakati za usiku.

Aidha, aliwashauri wamiliki wote wa kumbi na nyumba za starehe, baa na nyumba za ibada kujenga majengo ambayo yatakuwa yanazuia sauti isisafiri umbali mrefu na kusababisha madhara kwa wananchi wengine.

# GEL kuwaletea fursa wahitimu vyuo

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Global Education Link (GEL), imesema inatarajia kuleta fursa nyingi kwa vijana wanaomaliza vyuo katika maonyesho ya vyuo vikuu yaliyopangwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu.

Maonyesho hayo yanayotarajiwa kushirikisha zaidi ya vyuo vikuu 70 yameandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) na yanatarajiwa kufanyika kwa siku sita kuanzia Agosti 31, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Abdulmalik Mollel, alisema moja ya mambo watakayokuja nayo ni kuwaongoza vijana kusoma kozi zenye soko kwa wakati huo ili wakimaliza wapate ajira moja kwa moja.

"Sisi tunaangalia unakwenda kusoma nini na kama unachokwenda kusomea kina uhitaji gani na kwa kiasi gani kwa wakati huo mfano inawezekana leo kukawa na hitaji kubwa la wahandisi wa mafuta na gesi, lakini haina maana kwamba miaka mingine ijayo hitaji hilo likaendelea kuwapo kwa hiyo lazima tuwasaidie wanafunzi wasome kwa malengo," alisema Mollel.

Alisema hiyo inaweza kusababisha vijana wengi kwenda kusomea kozi ambazo zina watu wengi na hazina mahitaji makubwa kwa wakati husika hivyo kusababisha kuongezeka kwa tatizo la ajira nchini.

Alitaja jambo la pili ni ufuatiliaji na kushiriki naye fursa mbalimbali wanapokuwa nje ya nchi kimasomo, ili wanapohitimu na kuja nchini wawe na kitu chenye tija ambacho wanaweza kufanya na kujiingizia kipato badala ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema huduma nyingine itakuwa idara ya uwakala wa utoaji wa huduma za afya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutangaza huduma bora za afya zinazopatikana hapa nchini ili watu wa nje nao waje kutibiwa Tanzania kama Watanzania walivyokuwa wakienda kwao.

Alisema ndani ya idara hiyo watafungua dawati la ushirikiano na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi ambavyo vimeonyesha kiu ya kushirikiana kwenye nyanja mbalimbali za kitaaluma na GEL itakuwa kiungo baina ya vyuo hivyo, pia kwa vyuo vitakavyohitaji 'exchange program' za wanafunzi ama 'fellowship programs' basi huduma hizo zitasajiliwa hapo kwa watakaohitaji.

Alisema watakuwa na utoaji wa mikopo isiyo na riba kwa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi na kutakuwa na madawati maalum kwa wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma.

## PM asifu wajenzi wa kiwanda cha sukari

**Na Mwandishi Wetu,** BAGAMOYO

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesifu wajenzi wa Kiwanda cha Bagamoyo (BSL) kinachofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kwa shilingi bilioni 15, na kusema kukamilika kwa kiwanda hicho kutapungaza uagizaji wa sukari kutoka nje.

Akizungumza na wageni na wafanyakazi wa kiwanda hicho, Waziri Mkuu alisifu ujenzi wa kiwanda hicho na kusema: "Mahitaji ya sukari ya mezani kwa sasa hapa nchini ni tani 450,000, uzalishaji wetu ni tani 380,000. Tuna upungufu wa tani 70,000. Niwapongeze wawekezaji wanaojenga kiwanda hiki na taasisi zote za fedha kwa jitihada zilizochukuliwa mpaka kujengwa kwa kiwanda hiki. Kiwanda kikianza kufanyakazi tutaweza kukidhi mahitaji ya yetu ya ndani,'' alisema Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu aliwataka Watanzania kubadilika na kuanza kujivunia bidhaa zinazozalishwa nchini na kutokana na kasumba ya kuamini bidhaa za nje ni nzuri zaidi.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Bakhresa, Abubakar Bakhresa, mbali ya kumshukuru Rais Magufuli kwa kuwapatia shamba lenye hekta 10,000, ambalo watalitumia kuzalisha miwa na aliahidi kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuipeleka nchi kwenye uchumi wa viwanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema mbali ya kuwezesha kiwanda hicho, benki imelenga pia kuwanufaisha wakulima wadogo wa miwa.

## Shule yakana kutoza ada wakati wa corona

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

SHULE ya Msingi Tufiq Islamic iliyopo Maambani Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba imekanusha kuwadai wazazi ada za masomo kwa kipindi ambacho shule zilifungwa kutokana na ugonjwa wa corona.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Khamis Massoud, alisema hawajawadai wazazi ada kwa miezi ambayo skuli zilifungwa kutokana na ugonjwa wa corona.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mkuu huyo alisema kuwa, madai hayo yanayotolewa na wazazi sio ya kweli na kwamba hawajawahi kuwadai pesa ya ada kwa miezi hiyo na kwamba wanatekeleza agizo la serikali.

Alieleza kuwa, skuli hiyo inafuata maagizo yote yanayotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikiwamo hilo la kutowatoza wazazi ada za masomo kwa wanafunzi hao kipindi cha miezi ambayo skuli zilifungwa.

"Hatujawahi kuwadai wazazi ada ya kipindi ambacho skuli (shule) zilifungwa kwa kuwapo janga la Corona, tunafuata agizo la serikali na wanachotakiwa ni kulipa kwa mwezi uliopita," alisema.

Awali, baadhi ya wazazi waliilalamikia shule hiyo kuwadai ada ya masomo kwa miezi ambayo shule zilifungwa, jambo ambalo liliwatia wasiwasi hasa waliposikia agizo la serikali la kutotozwa ada kwa wazazi.

## Fursa kwa wakulima miwa wa Kilombero

**Na Gwamaka Alipipi**

UONGOZI wa kiwanda cha sukari Kilombero, umeingia mkataba wa mwaka mmoja na wakulima wa miwa wa Wilaya ya Kilombero kuanza kununua miwa.

Akizungumza baada ya kuingiwa kwa mkataba huo, Meneja Uendelezaji wa wakulima wa miwa wa kiwanda hicho, Job Zahoro, alisema wameendelea kuwa na mikataba na wakulima kila baada ya miaka mitatu, kunakochangiwa na kampuni kutambua thamani ya wakulima hao.

Alisema wakulima wa miwa Wilaya ya Kilombero wanachangia asilimia 45 ya malighafi msimu mzima katika kampuni hiyo.

Zahoro alisema uongozi wa kiwanda kwa kutambua thamani hiyo, waliamua kuwa na mkataba na wakulima utakaokuwa unaratibu mambo mbalimbali ikiwamo, kiasi gani cha miwa ingia kiwandani, ubora wa miwa na bei.

Aliongeza kuwa uongozi wa kiwanda kwa kushirikina na viongozi wa vyama vya ushirika, wamesaini mkataba huo wa ugavi wa miwa, ili baada ya malengo ya kupanua kiwanda yatakapokamilika mkataba wa muda mrefu kuhusisha mahitaji yote.

"Baada ya mkataba huu wa mwaka mmoja kumalizika ambao ni mwendelezo wa mkataba ulioisha, tutapata nafasi ya kujadili changamoto ya mabadiliko ya teknolojia na mabadiliko ya upanuzi wa kiwanda," alisema Zahoro.

Mkuu wa Idara ya Wakulima Kilombero, Hans Veenstra, alisema katika mkataba huo wa muda mfupi, kuna kanuni na taratibu zinazoainisha namna ya uendeshaji katika kazi za kila siku.

Alisema kanuni hizo zinawahakikishia wakulima kuwa kiwanda cha sukari Kilombero kimejiandaa kuendelea kuimarisha mahusiano yalipo baina yao, kama wadau muhimu katika uzalishaji wa sukari.

Aliongeza kuwa kiwanda kinaweka jitihada za makusudi kuhakikisha mkataba huo unaendelea kuainisha mambo ya msingi ambayo ni mazuri.

Mmoja wa wakulima hao, Jitihada Yusuph, akizungumza na Nipashe alisema amefurahishwa na mkataba huo kutokana na kuwa na manufaa kwa wakulima na kuonyesha dira ya utendaji kazi, uhakika wa kuuza miwa wanayozalisha pamoja na soko la uhakika baada ya mavuno.

Alisema: "Leo tumesaini mkataba wa kuingiza miwa kiwandani, mkataba huu huwa tunaufurahia sana kwa kuwa una manufaa kwetu, manufaa tunayoyapata lazima mwenye kiwanda atachukua miwa yetu."

# Corona yakwamisha ujenzi mradi wa maji

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MLIPUKO wa virusi vya corona umetajwa kuchangia kuchelewa kukamilika kwa mradi wa maji kutoka Mji wa Kahama kwenda Kata ya Mondo katika halmashauri ya mji huo.

Hiyo inatokana na viwanda vingi vya nje kusimamisha uzalishaji wa malighafi na hivyo kusababisha vikwazo katika ukamilikaji wa ujenzi wa mradi huo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (KUWASA) ikitegemea kupata vifaa hivyo mwezi ujao.

Juzi, Kaimu Mkurugenzi wa mamlaka husika, Magige Marwa, alimweleza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, aliyekuwa akikagua mradi huo kuwa unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 445. Alisema fedha zinazotumika kutekeleza mradi huo ni za mapato ya ndani ya mamlaka hiyo kwa asilimia 100, ukjitarajiwa kuwanufaisha wananchi na viwanda vinavyotarajiwa kujengwa eneo hilo.

Marwa alibainisha kuwa mpaka sasa, mradi huo umegharimu Sh. milioni 262.6 na haitachukua muda mrefu kuukamilisha ili kusogeza huduma ya majisafi na salama katika Kata ya Mondo viliko viwanda vya kimkakati vinajengwa vya Kampuni ya Kahama Oil Mills (KOM). Alisema mradi huo pia utanufaisha shule na zahanati, huku ukitegemea kuwatua ndoo kinamama na kuongeza mapato kwa mamlaka.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga (Telack), alisema lengo la serikali kutekeleza mradi huo ni kusogeza huduma za kijamii kwa wananchi ili wawe na uhakika wa kuzipata muda wote.




Mwenyekiti wa Wakulima Bonde la Kilombero, Bakari Mkangamo (kushoto) na Mkuu wa Idara ya Wakulima wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Hans Veenstra, wakionyesha makubaliano ya mkataba wa mwaka mmoja uliosainiwa kati ya wakulima wa miwa wa bonde hilo na kampuni hiyo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanahabari wafundwa kulinda taaluma

**Na Happy Severine,** SIMIYU

KAIMU Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Khamis Kulemba, ameitaka klabu ya waandishi wa habari Mkoa wa Simiyu kutomwonea aibu na kumchukulia hatua za kinidhamu mwandishi yeyote atakayekiuka maadili na taratibu za kazi zao.

Alisema lengo la kuchukua hatua dhidi ya watakaokiuka ni kudhibiti ni kulinda taswira ya taaluma ya uandishi wa habari.

Dk. Kulemba aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya magonjwa ya mlipuko kwa wanahabari wanachama wa klabu ya waandishi mkoani Simiyu yaliyofanyika Mjini Bariadi chini ya ufadhili wa Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

Alisema waandishi wa habari wa Mkoa wa Simiyu wamekuwa wakijituma na kufanya kazi zao ipasavyo, hivyo ni vema wakawa makini kuendelea kusimamia maadili yao na isije kutokea mmoja wao akachafua taswira nzuri iliyojengwa kwa miaka mingi.

"Nipende kutoa rai kwa waandishi wa wote, zingatieni kanuni na maadili yanayoongoza katika kufanya kazi zenu... asitokee mmoja akaenda tofauti na kuchafua taaluma nzima," alisema Dk. Kulemba.

Ofisa Habari kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu, Sarah Kibonde, alisema msingi bora wa mwandishi wa habari ni kufuata maadili, sheria, kanuni kwa mujibu wa sheria ya huduma za habari inavyoelekeza ili kutekeleza majukumu yao salama.

Aidha, aliwasihi waandishi wa habari ambao hawajajiendeleza kimasomo kama ambavyo sheria inavyowataka ya kuwa na elimu kuanzia stashahada, wakasome ili sheria hiyo isije ikawapitia.

Awali akizungumzia juu ya magonjwa ya mlipuko kwa waandishi wa habari waliotembelea Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi (Somanda), Kaimu Mganga Mfawidhi, Dk. Nyangi Thomas, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikisumbuliwa na magonjwa ya mlipuko ambayo wamekuwa wakiwaathiri zaidi watoto wadogo.

ama
ALHAMISI AGOSTI 27, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Wanawake waeleza athari janga la corona**



Ukurasa 12

Taathiri ya ubakaji ilivyochangia kumletea ugumba binti miaka14



Ukurasa 14

**Chunga, kucheua ni hatari afya ya koo kwa watu wazima**

MAZINGIRA

# KUDHIBITI TABIANCHI

• Mitungi gesi kilo 2 yafika vijijini • Gesi asilia yasambazwa pia

**Na Jenifer Gilla**

KWA Tanzania hakuna mpinzani wa mkaa na kuni kwenye kupikia iwe nyumbani na kwenye sherehe. Kwanza zote zipo 'faster'", anasema Rose Paschal, huku akifuta macho yaliyojaa machozi yaliyosababishwa na moshi unaotoka kwenye jiko la kuni alililokuwa akipuliza.

Rose anatoa majibu hayo kwa mwandishi wa Nipashe walipokutana kwenye sherehe kwa jirani yao, ambapo kuni pekee zilitumika kupikia hivyo kusababisha moshi kutanda katika eneo hilo.

Mama huyo mwenye familia yenye watoto watatu anayeishi Tabata Segerea, anazidi kueleza kuwa akiwa nyumbani, anatumia mkaa kwa vile ni nafuu.

Akiwa na kipato cha Sh. 380,000 kwa mwezi anasema hajui nishati nyingine badala ya mkaa na kuni tena hajawahi kutumia gesi kwa madai kuwa gharama zake ni kubwa na hicho ndicho kikwazo kwake.

"Natamani kutumia gesi lakini nina familia kubwa siwezi maana mtungi mkubwa wa kilo 28 unaofaa kwa familia unauzwa Sh.50000, ambao naweza kuutumia mwezi mmoja tena kupikia vyakula vyepesi tu. Nikinunua gunia la mkaa la Sh. 40,000 natumia miezi miwili hii ni nafuu zaidi," anasema Rose.

Desteria Martin mfanyabiashara wa samaki wa kukaanga, anasema anatumia kuni kwenye biashara yake kwa kuwa ni nafuu na inaharakisha upishi wake. Anasema mtaji wake ni mdogo hivyo analazimika kubana matumizi kwenye moto ili aweze kupata faida.

"Ukaangaji wa samaki ni aidha utumie kuni au gesi kwa sababu wanakuwa wengi hivyo wanahitaji moto unaowaka sana ili wasinyonye mafuta mengi" anasema Desteria na kuongeza:



Mizigo ya kuni ikiandaliwa kwa ajili ya kwenda kuuzwa kwa matumizi ya kupikia. **PICHA: MTANDAO**

> **Mfano mtungi wa kilo 28 ni Sh. 50,000 bei yake haijabadilika kwa muda mrefu na hata ukija Dodoma utakuta bei ni hiyo hiyo, ndiyo maana halisi ya bei nafuu.**

"Sasa ukitumia gesi ni hasara mwisho wa siku faida huioni kwa hiyo hapa nikinunua fungu la kuni la Sh. 2,000 naongeza na vifuu inatosha kabisa kupikia samaki wa Sh. 40,000."

Hawa ni baadhi ya wateja wanaofikia asilimia 70 ya wakazi wa jijini Dar es Salaam, wanaotumia nishati isiyo salama katika kupikia, kwa mujibu wa Ripoti ya Matumizi ya Nishati Afrika ya mwaka 2019.

**GESI VIJIJINI**

Hata hivyo, mazoea haya yanaelekea kufikia ukingoni, serikali imeanza jitihada za kufikisha gesi vijijini ili kuwafikia wenye kipato kidogo kwa gharama nafuu.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (UWURA), Titus Kaguo, anazungumzia mpango wa serikali kupunguza matumizi ya nishati isiyosalama kupikia kwa kuhamasisha matumizi ya gesi ya mitungi LPG (Liquefied Petroleum Gas), vijijini kazi inayofanywa na EWURA.

"Nasema uhamasishaji huo pamoja na kuweka mazingira mazuri na fursa za biashara vimezaa matunda kwani wamepata wafanyabiashara wengi ambao hupeleka gesi ya bei nafuu mikoani.

"Sasa tuna wafanyabiashara wanaotengeneza mitungi midogo ya gesi ya kuanzia kilo mbili inayouzwa Sh.6, 000, gharama ambayo hata mtu wa hali ya chini anaweza kuimudu,"anasema Kaguo.

Kwa mujibu wa msemaji huyo wa EWURA, matumizi ya gesi ya LPG yameongezeka kutoka lita 6,000 mwaka 2008 hadi kufikia lita 145,000 Juni, 2019 hali inayoonyesha kuwa kuna muitikio mkubwa.

Anasema siri ya mafanikio hayo pamoja pia inahusisha kuzingatia ubora wa bidhaa na kuwapo gharama ambazo hazimuumizi mtumiaji na muuzaji na pindi wanapoona upande mmoja unaumia wanaingilia kati.

Akiongelea malalamiko ya gharama kubwa ya nishati hiyo, Kaguo anazikubali akisema ni za kawaida ndio maana hazibadiliki mara kwa mara tofauti na nishati nyingine.

"Mfano mtungi wa kilo 28 ni Sh. 50,000 bei yake haijabadilika kwa muda mrefu na hata ukija Dodoma utakuta bei ni hiyo hiyo, ndiyo maana halisi ya bei nafuu", anasema.

**GESI ASILIA**

Katika jitihada za kuwapatia wananchi nishati salama Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) linanajenga mitambo ya kusafisha gesi asilia ambayo imewekwa katika maeneo kadhaa nchini.

"Baadhi ya maeneo yaliyofikiwa na gesi hiyo ni Madimba (Mtwara) ,Songo Songo (Lindi) pamoja na Bomba la kusafirisha gesi asilia hiyo kutoka Mtwara, kupitia Somanga Fungu mkoani Lindi, Pwani hadi Dar es Salaam", anasema Marie Mselemu, Mkuu wa Habari na Mawasiliano wa TPDC

Kwa jijini Dar e salaam wakazi wa maeneo ya Ubungo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam(UDSM), Survey, Makongo juu, Samnujoma, Shekilango, Sinza, Mikocheni -Coca-Cola na Mwenge, wameanza kunufaika na gesi hiyo ambayo imeunganishwa kwenye nyumba zao kwa kutumia mabomba maalum.

"Lengo la serikali ni kufikisha gesi asilia, mbali na matumizi mengine inatumiwa kupikia nyumbani ili kupunguza matumizi ya kuni, mkaa na nishati zisizo salama kwa afya na athari za mazingira na gharama ," anasema Mselemu.

Kwa mujibu wa maelezo yake mradi huo utasaidia pia utunzaji wa mazingira unaotokana na kutatwa miti kwa ajili ya nishati ya kupikia ambayo kwa kiasi kikubwa inaathiri mazingira na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

**GHARAMA NAFUU**

"Gharama ya gesi hii ni Sh.1, 000 kwa uniti ambapo hata mtu wa kipato cha chini anaweza kuimudu. Familia ya watu sita wanatumia uniti moja tu kwa siku sawa na Sh.30, 000 mwezi," anasema Marie.

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Taathira ya ubakaji ilivyochangia kumletea ugumba binti miaka14




Maofisa wa shirika la SPRF wakiwa na familia ya binti aliyefanyiwa ukatili wa kijinsia, kijijini kwao Mangaa Ikungi, wakipanga mipango ya kusaka haki iliyoporwa. **PICHA:DOTTO MWAIBALE**

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

"NIKIWA darasa la saba nilibakwa nikapata ujauzito, Nikafukuzwa shule. Nikakaa nyumbani hadi nilipojifungua. Nilipata wakati mgumu mno kipindi chote cha ujauzito na wakati wa kujifungua ililazimika nifanyiwe upasuaji nikajifungua salama lakini kizazi changu kiligundulika kuwa na matatizo hivyo kiliondolewa...Hapa sina tena kizazi, mfuko wa kizazi umeondolewa nikiwa mtoto wa miaka 14. Na hizo huenda ni athari za kubeba mimba katika umri mdogo."

Ni kisa mkasa cha binti wa miaka 14, aliyekuwa mwanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Msingi Mungaa mkoani Singida, jina linahifadhiwa.

Anakumbuka zaidi: "Nilizibwa mdomo na kukandamizwa kwa nguvu shingoni, anayenibaka alikuwa na panga, akanitisha nikithubutu kupiga kelele ananikata shingo, sikuwa na msaada alinibaka...nashindwa kusimulia uchungu na maumivu makali niliyoyapata."

Alinyanyaswa Januari 2019 akiwa anarudi nyumbani akitokea shuleni, mwendo wa takribani nusu kilometa baada ya masomo jioni. Anasema, ghafla kati ya njia alikutana na kijana mmoja anayeishi kijijini hapo na anayemfahamu.

> **"Nikiwa njiani huku nikilia kwa uchungu nilijiuliza nitaanzaje kuwaeleza wazazi? Na vipi endapo nitapata ujauzito? Na je, kuhusu hatma yangu ya masomo itakuwaje?**

Kijana huyo ambaye naye (jina limehifadhiwa) alianza kumtomasa na kumvuta kwa nguvu na kumnyonga mikono ili kumtoa njiani hadi alipomfikisha eneo ambalo hapakuwa na watu.

"Nilibaki nikitetemeka na kujikuta nikiishiwa nguvu, sikuweza tena kupiga kelele wala kulia kwasababu nilielekezewa panga.Nikajikongoja kwenda nyumbani huku nikiwa nimechafuka kwa mengi, kuanzia moyoni hadi mwilini," anaeleza mhanga wa tukio hilo.

Anasema: "Nikiwa njiani huku nikilia kwa uchungu nilijiuliza nitaanzaje kuwaeleza wazazi? Na vipi endapo nitapata ujauzito? Na je, kuhusu hatma yangu ya masomo itakuwaje? Kwa kweli nilichanganyikiwa sana unyama ule uliniumiza, lakini baada ya kupita miezi 4 kila kitu kilikuwa wazi. Ni ujauzito."

### KUFUKUZWA SHULE

Kama alivyotabiri binti, siku ile ya tukio ndivyo ilivyotokea alipata ujauzito na akiwa shuleni alionekana mjamzito na Mwalimu Mkuu aliandika barua kuwaita wazazi wake baada ya kukamilisha hatua zote za kumchukua vipimo, ambavyo vilithibitisha kitaalamu.

Anasema wazazi wake walifika shuleni na kuelezwa mabadiliko walioyaona kwa binti huyo na hatimaye walijulishwa kwamba ni mjamzito, na kwa mujibu wa taratibu za shule hiyo hataweza tena kuendelea na masomo, hivyo warudi naye nyumbani.

Amepata mtoto kwa njia ya upasuaji lakini kizazi kimeondolewa katika umri mdogo na anasema kinachomuumiza zaidi ni pale anapomuona mshitakiwa aliyemfanyia ukatili ule akiwa huru mtaani na anaishi kwa furaha bila msaada wala habari yoyote, hakuna hatua yoyote aliyochukuliwa mpaka sasa licha ya tukio kuripotiwa polisi, na baadaye shauri hilo kupelekwa Mahakama ya Mwanzo Utemini mjini Singida.

### KUPIGWA DANADANA

"Baada ya kesi hii kuripotiwa kituo kidogo cha polisi katika Kijiji cha Mungaa na baadaye kupelekwa mahakamani Utemini mjini Singida, kila shauri lilipokuwa likitajwa mahakamani tulijikuta tukihudhuria mimi na wazazi wangu. Mshitakiwa alikuwa hafiki wala haonekani. Kwa kweli ilifika wakati na sisi tukaishiwa nauli tukashindwa kuhudhuria hii kesi kila ilipokuwa ikitajwa," anasimulia binti huyo.

Anasema mpaka kufikia Februari 4 mwaka huu, shauri hilo lilikuwa halijatolewa hukumu na mshitakiwa yuko huru mtaani huku msichana huyo aliyekatizwa masomo akiwa tayari amepoteza mwelekeo na ndoto zake karibu zote za kuendeleza maisha yake akiendelea kusota.

### SPRF ILIVYOMUIBUA

"Kwasasa nafanya biashara ya kuuza kuni ninazozitafuta mbali natembea kilometa tatu kutoka hapa nyumbani hadi porini huku nikiwa na mtoto wangu mgongoni. Nafanya hivi ili kutafuta pesa za kunisaidia kumtunza mwanangu. Nauza kuni kwa Sh. 2,000 kwa fungu moja," anasimulia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la JIOKOE na UMASKINI 'SPRF' - Stars of Poverty Rescue Foundation, Dk. Suleiman Muttani,anasema katika kutekeleza mradi wa AWARE, walitoa taarifa ya tukio hili.

Muttani na watendaji wenzake kupitia kikundi cha elimu na hamasa cha mradi wa AWARE dhidi ya matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, maarufu 'Sauti ya Mwanamke' katika Kijiji cha Mungaa, anasema ndipo walipoibua sakata hilo.

Hata hivyo, Muttani anasema kazi bado ipo wanaendelea kuwasiliana na maofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Ikungi, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya kisheria vinavyoshughulikia shauri hilo ili kumsaidia mwathirika apate haki yake na mshitakiwa pia aone haki ikitendeka.

"Mbali na matukio mengine ya aina hii, mpaka sasa shirika letu limeibua mikasa ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii takribani 56 yakiwemo masuala ya ubakaji, vipigo kwa wanawake na watoto, mimba na ndoa za umri mdogo na mengine ambayo chimbuko lake ni imani za kishirikina sanjari na mila na desturi zilizopitwa na wakati ambazo zinakatishwa na wakati ambao ukeketaji ambao kwa sasa unafanywa kwa siri kubwa kwa watoto wachanga usiku wa manane," anasema Dk. Muttani.

## Kudhibiti tabianchi

**INATOKA UK.11**

Jitihada hizo zinakuja, wakati ripoti ya Matumizi ya Nishati Afrika ya mwaka 2019 inasema asilimia 70 ya wakazi wa Dar es Salaam, wanaotumia nishati isiyo salama katika kupikia .

Inaieleza pia Tanzania yenye watu milioni 56, ina matumizi makubwa nishati isiyo salama ikiongozwa na kuni, pumba kwa asilimia 66 na mkaa asilimia 27 wakati asilimia tano pekee ndiyo hutumia gesi.

Hata hivyo, juhudi mbalimbali zinafanyika kuhakikisha kuwa kufikia mwaka 2030 matumizi ya nishati isiyosalama katika kupika yanashuka kwa kiwango cha nusu kutoka asilimia 66 hadi 33 kama malengo ya Sera ya Mazingira.

### MAONI YA WADAU

Desteria Kamugisha, mkazi wa jijini Dar es salaam, ni mtumiaji wa gesi ya LPG ya kilo 15 inayouzwa Sh.50,000 na hudumu kwa miezi miwili na nusu.

Kwa mujibu wa mama huyu mwenye familia ya watu wanne, anatumia gesi kwa sababu ni salama kwa afya na hurahisisha mapishi.

Hata hivyo, anasema kuwa ili adumu na nishati hiyo kwa muda mrefu inamlazimu kununua mkaa ili kupikia vyakula vinavyochelewa kuiva kama vile maharagwe na makande.

"Kama ningekuwa napikia hadi maharagwe au kande nadhani ingedumu wiki chache kwa kuwa hapa kwetu tunapika mara tatu kwa siku, inabidi ninunue na gunia la mkaa ili kuchanganya", anasema Desteria .

Maria Dama, mkazi wa Mikocheni Dar es salaam anasema ameona unafuu wa maisha katika kupikia tangu aanze kutumia gesi ya asilia inayosambazwa na TPDC.

Anasema inamgharimu Sh. 25,000 hadi 30,000 kulipia gesi hiyo kwa mwezi kulingana na ugumu wa chakula anachopika tofauti na zamani ambapo alikuwa akitumia gesi ya mtungi wa LGP ambao alikuwa akilipia Sh. 50,000 hivyo gharama imepungua karibu nusu.

AFYA

# Wanawake wapaza sauti athari za janga la corona

**Na Daniel Eliewaha**

MAGONJWA kama malaria, Ukimwi, ebola, saratani na surua yamesumbua watu kwa miaka mingi na kusababisha vifo vingi. Lakini ugonjwa mpya wa virusi vya corona (COVID-19) ulioanza kujitokeza China mwishoni mwa mwaka jana na kusambaa nchi nyingi duniani mwanzoni mwa mwaka huu umezua tafrani kubwa.

Takwimu zilizotolewa kwenye vyombo vya habari vya kimataifa Agosti 20, mwaka huu, zinaonyesha kuwa watu walioathirika duniani hadi siku hiyo ni milioni 22.7 na vifo vilikuwa 794,000. Kwa maana hiyo, ugonjwa huu ni tishio kubwa kwa kuzingatia kuwa umesambaa kwa kasi kwa miezi sita tu tangu Machi, mwaka huu.

Baadhi ya wananchi, hasa kinamama na wasichana kwenye maeneo kadhaa jijini Dar es Salaam yakiwamo Tegeta, Wazo Hill, Kunduchi na Ununio walihojiwa hivi karibuni juu ya yale waliyoyaona kwenye kipindi hicho. Jumla ya wanawake na wasichana 47 walihojiwa kuhusu janga hilo.

Tatizo kubwa, walisema lilikuwa la kuzuiwa kutoka kwenda kwenye biashara na shughuli zao za kila siku zinazowapatia riziki zao, hivyo kubaki majumbani wakiwa wamejifungia.

Zainabu Almasi (58), mkazi wa Wazo Hill anayeuza chakula Tegeta Sokoni, alisema kwa kuwa corona ilikuja bila taarifa, yeye na wenzake hawakuwa wamejiandaa. Anasema kati ya Machi na Juni, kipato chake kiliporomoka, kwanza, kwa sababu wateja wake walipotea na pia alikuwa hawezi kufika kila siku kwenye meza yake ya biashara.

Hatua hiyo, anasema ilisababisha kula hata mtaji wake wa kununulia chakula kwa ajili ya biashara kwa maana ya mchele, unga, sukari, mafuta ya kupikia na viungo.

Khadija Ulanga, ambaye ni mama lishe, naye alikiri kuwa corona ilisababisha kuishiwa fedha kwa sababu wateja wake wengi walipotea na wengine akikutana nao walimuambia "janga hili linapenda mtu aache tabia ya kulakula kila wakati".

Tutindaga Mwakipesile (38) anayeishi Boko ambaye hufanya kazi ya kuuza vyakula na kupamba wakati wa sherehe na misiba, alisema biashara hiyo iliporomoka katika kipindi cha janga la corona.

"Huwezi kuamini nilikuwa na wasichana tisa nafanya nao hizo kazi ilibidi kuwaachisha kazi kwa sababu tulikuwa hatupati tenda tena kwa kuwa shughuli hizo zilisitishwa rasmi na serikali kuzuia mikusanyiko ya watu", alisema.

Hata hivyo, anamshukuru Mungu kuwa kuanzia mwezi uliopita hali imebadilika na baadhi ya wateja wanampigia simu kutaka waonane.

Anita Laizer (27) akiwa na mama yake mkubwa Linda Mollel (66) wanaoishi Kunduchi, wote walikiri



Mamalishe akiandaa ugali kwa ajili ya mlo wa mchana kwa wateja wake, katika eneo la Mburahati kwa Jongo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOHN BADI**

> **Wahudumu waliokutwa kwenye baa hizo walisema wamerudishwa kazini mwanzoni mwa mwezi huu baada ya kuanza kuongezeka kwa wateja.**

kuwa kipindi chote cha corona kilikuwa na changamoto nyingi ikiwamo kutoshikana mikono, kuvaa barakoa wakati wote na kubugia maji ya moto ya tangawizi na limao, licha ya kujifukiza na mchaichai huku wamejifunika blanketi.

Laizer alisema kilichomshangaza ni wazazi ambao walikuwa wanawaacha huru watoto au vijana wao waliorudi nyumbani toka shuleni na vijana hao wa kike na kiume wakaishia kuchezeana na kufanya mapenzi bila kinga wala kuogopa ukimwi.

"Sijui maadili yaliyozoeleka zamani yameenda wapi. Jioni kuna vijana wa kiume tunawajua walikuwa wakiingia kwenye nyumba moja inajengwa na kufanya mapenzi tena wa jinsia moja. Watoto wa kike walikuwa wanapewa Sh. 1,000 au 2,000 na kuingizwa kwenye vyumba vya vijana wasio na kazi na kufanyiwa michezo michafu. Tunafurahi wanafunzi walirudi shule kwani ilikuwa balaa mitaa tunayoishi," alisema Mollel kwa uchungu.

### KILIO WENYE BAA

Athari nyingine iliwakumba wenye baa waliohojiwa katika maeneo ya Bunju A na B, zile zilizoko barabara ya Bagamoyo kuhusu ukosefu wa wateja hadi baa zingine kufungwa. Baa nyingi kwenye maeneo hayo zilifungwa sasa zinakarabatiwa ili 'zirejee kazini'.

Wahudumu waliokutwa kwenye baa hizo walisema wamerudishwa kazini mwanzoni mwa mwezi huu baada ya kuanza kuongezeka kwa wateja.

"Si unakumbuka hata kabla ya corona watu walipungua sana kwenye baa kwa sababu hawana pesa ya kununulia konyagi, bia na mvinyo. Walikuwa wananunua chupa za maji na kugawana. Sasa corona ndiyo ikafanya hali kuwa mbaya zaidi ikabidi tufukuzwe kazi", alisema Pili Mkuchika huku akibainisha kuwa wahudumu wengi waliachishwa kazi kwenye baa zilizoko Bunju.

Hiyo hali ya ukosefu wa wateja kwenye baa Tanzania ni tofauti na Afrika Kusini ambapo Julai 13, mwaka huu, serikali ya nchi huyo ilipiga marufuku uuzaji wa pombe kwenye maduka na baa kutokana na ulevi kuongezeka wakati wa COVID-19.

Watu wengi nchini humo wanadaiwa wameongeza ulevi kutokana na mazingira ya kuachishwa kazi na kuambiwa wakae nyumbani jambo ambalo hawakuwa wamezoea. Hospitali zilijaa watu kwa sababu ya ulevi huku vitanda vikihitajika kuwalaza wenye corona, hivyo ikaonekana ni vizuri pombe zipigwe marufuku.

Wanafunzi wa kike na wa kiume nao wana mambo mengi waliyojifunza wakati wa corona, lakini baadhi walilalamika kufanyishwa kazi nyingi walipokuwa nyumbani hata wakashindwa kusoma kikamilifu.

Wengine wanalaani vitendo vya madereva na makondakta wa daladala kuwaacha vituoni kwa visingizio mbalimbali, hivyo kuwafanya wachelewe shuleni asubuhi na jioni wakati wakirudi nyumbani.

"Hawa makondakta hawatupendi. Unaweza kukuta asubuhi daladala haina watu lakini wanafunzi tunapoikimbilia wanatukwepa au katika wanafunzi 10 watachukua wawili tu," alisema Martha Mnzava aliyekutwa katika kituo cha basi cha Kibo Complex, Tegeta.

Madereva na makondakta walisema bado serikali haijatoa ufafanuzi kuhusu kujaza watu kwenye mabasi kwa kuwa miezi michache iliyopita walikataza misongamano ya watu kwenye magari ya umma.

Baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa walisema waliwahi kusikia mara nyingi kesi na watoto wa shule kubakwa wakati COVID-19 ilipopamba moto pamoja na ukatili wa kijinsia lakini halikuwa na nguvu kubwa kwa wanafamilia waliyamaliza wenyewe bila kuyaripoti polisi au serikali za mitaa ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Baadhi ya kinamama waliiomba serikali kushughulikia kwa makini tatizo la ajira kwa vijana wa kiume na wa kike wakiogopa kuwa wengi wamejiingiza kwenye umalaya wa chini kwa chini ili wapate pesa ya kujikimu. Walisema vijana wengi waliomaliza darasa la saba na sekondari wanazurura kuanzia asubuhi na kufanya mambo yasiyo na maadili.

Mkurugenzi Mkuu wa Women Fund Tanzania -Trust (WFT-T), Mary Rusimbi, alisema mfuko wake utaendelea kutoa ruzuku kwa mitandao na vikundi vya wanawake na watoto ili kupambana na athari za corona ikiwamo hali ngumu ya kiuchumi, ukatili wa kijinsia, mfumo dume, rushwa ya ngono na mambo mengine ambayo huwaathiri zaidi wanawake.

AFYA

# Chunga, kucheua ni hatari afya ya koo kwa watu wazima




Mgonjwa akichunguzwa saratani ya njia ya chakula. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KUCHEUA ni michakato ya kumeng'enya chakula iliyozoeleka kwa watoto wachanga, lakini kwa watu wazima si jambo salama kiafya.

Ni kwa kuwa kucheua hurudisha chakula pamoja na vimeng'enyo vyenye tindikali na nyongo kwenye njia ya kupitisha chakula na kooni na kusababisha uwezekano wa kupata saratani kwenye njia ya chakula.

Zama hizi saratani ni changamoto kiasi kwamba kuna hofu zaidi mtu anapogundulika kuwa ana saratani kuliko pengine akiambiwa ana tatizo la virusi.

Changamoto ya saratani ni kushambulia kila kiungo kuanzia seli za damu, viwanda vya kuzalisha damu ndani ya mifupa au uroto, ini ,kizazi na tezi dume. Hizo ni baadhi ya saratani zinazohofisha wengi na kukatiza maisha yao.

Jamii nyingine ya saratani ni kansa ya koo seli za kiungo hicho zinabadilika, kuasi na kugeuka kuwa saratani na wakati mwingine hujitokeza kwenye maeneo kama kidaka tonge, kisanduku cha sauti na kwenye matezi ya kooni.

> **"Chembe hai hizo au seli za eneo hilo ambalo lina kidaka tonge, boksi la sauti na tezi mbalimbali hubadilika na kuasi na kuwa kansa.**

Swali ni nini kinachosababisha? Viashiria vyake vya hatari ni vipi? Dalili , vipimo, matibabu na mategemeo yake.

Mategemeo ni jambo la mwisho yaani nini kitatokea baada ya kuugua saratani kwa kitaalamu wanaelezea kama 'prognosis' kwamba mgonjwa akishagunduliwa anaumwa saratani fulani ni nini hatma yake.

Kwa mfano anaweza akaishi miaka mingapi zaidi na maisha yake yakawa yameathirika kiasi gani? Je, aina hiyo ya maradhi uponaji wake ukoje kwa kuangalia asilimia za wanaogundulika na kupona kuanzia watoto hadi watu wazima.

Katika kuangalia maradhi hayo njia ya chakula, wapo wanaoiita kansa ya koo au ya koromeo, pengine ukweli ni kwamba ni njia ya kumezea na kupitisha chakula.

Njia hiyo ni kama mrija (tube) wenye urefu wa kama inchi nane unaopeleka chakula kutoka mdomoni mpaka tumboni.

Unapomeza chochote misuli ya mrija huu inagandamiza na kusukuma ili kukifikisha tumboni. Mwishoni mwa mrija huu pale unapoingia tumboni kuna 'valvu' au kifuniko kinachojifungua kuruhusu chakula kiingie tumboni na kujifunga ili kisirudi nyuma kwenye njia ya kumeza chakula na kupanda tena juu.

Saratani ya njia ya kumeza chakula huanza kwenye seli zinazogusana moja kwa moja na chakula au chochote binadamu anachomeza.

Chembe hai hizo au seli za eneo hilo ambalo lina kidaka tonge, boksi la sauti na tezi mbalimbali hubadilika na kuasi na kuwa kansa.

Saratani isipodhibitiwa inakua haraka na kusababisha uvimbe ambao unaweza ukaendelea kukua na kubaki kwenye njia ya kumeza chakula au kuhamia sehemu nyingine za mwili kwa kupitia kwanza kwenye kuta za kiungo hiki au kwenye damu na maji ya tezi kuelekea kwenye matezi na viungo vingine jirani kama mapafu, ini, tumbo au hata kwenye ubongo na mifupa.

## KUCHEUA KUNACHANGIA

Saratani ya njia ya kumeza chakula hutokea kwenye seli zilizokaribu na kiungo hiki kinapoingia kwenye tumbo kwenye'glanduar cells' .

Glandi ni kiungo kinachotengeneza kichocheo kinachoingia moja kwa moja kwenye damu au viungo vingine kupitia kwenye mrija (tube) unaoounganyisha viungo viwili.

Seli za glandi zilizopo kwenye njia ya kumeza chakula zinatengeneza ute unaolainisha njia ya kumeza chakula ili kipite kwa urahisi.

Saratani hii ya 'adenocarcinoma' hutokea zaidi kwa watu wanaocheua mara kwa mara hali inayoitwa kwa kitaalamu 'chronic regurgitation' Mtu anapocheua yaani chakula ambacho kimeishaingia kwenye tumbo na kuchanganyikana na tindikali humo tumboni kinarudi kwenye njia ya kumeza chakula. Tindikali hii inapotoka tumboni na kurudi kwenye njia ya kumeza chakula huziharibuseliza glandi zilizopo eneo hili chini ya njia ya kumeza chakula na kuzisababishia kugeuka ziwe za saratani.

## AINA NYINGINE

Zipo aina mbili za saratani ya njia ya kumeza chakula kutegemea na seli zinazobadilika na kuwa saratani ambazo ni za aina mbili zinazoitwa kwa kitaalamu 'squamous cells' na 'glandular cells' saratani itokanayo na 'squamous cells' inaitwa 'Squamous cells carcinoma' na itokanayo na 'glandular cells' ni 'adenocarcinoma.

'Squamous cells carcinoma' hutokea kwenye sehemu ya juu kama katikati ya njia ya kumeza chakula. Hii ya pili yaani 'adenocarcinoma' hutokea pale njia ya kumeza chakula inapoingia kwenye tumbo.

## VISABABISHI

Kama saratani nyingine, chanzo cha hii hakieleweki vizuri lakini kuna viashiria vya hatari vilivyoonekana kwenye sehemu nyingine. Kwa mfano huko India saratani hii huonekana sana katika jimbo la Kashmir ambalo watu wake wanakunywa kwa wingi chai chungu inayoitwa 'noon chai' Tabia nyingine za watu wa Kashmir zinazohusiana na saratani hii ni kula vyakula vyenye viungo vingi kama pili pili, mafuta mengi na kuvuta sigara . Vyakula na vitu hivi vinakereketa seli za usoni mwa kiungo hiki cha kumezea chakula na baada ya muda mrefu kusababisha ugonjwa huo.Vingine ni kuvuta sigara,

## MITANDAO YA SARATANI



# Jumuiya yamuunga mkono JPM kwa mil. 40/- ujenzi wa msikiti

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JUMUIYA ya Maridhiano ya Taifa imetoa Sh. milioni 40, kwa ajili ya kumuunga mkono Rais John Magufuli kujenga msikiti wa Chamwino mkoani Dodoma.

Pia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), limeshapeleka vifaa kwa ajili ya kuanza ujenzi haraka iwezekanavyo.

Mchango huo ni mwendelezo wa harambee iliyofanyika chini ya Rais Magufuli katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Emmaculata Jumapili iliyopita kwa ajili ya ujenzi wa msikiti huo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema anaishukuru jumuiya hiyo kutokana na mchango waliotoa kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa msikiti huo.

Fedha hizo ambazo zimekabidhiwa kwa Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Charles Mbuge, ambaye aliahidi kuzifanyia kazi na kukamilisha ujenzi huo haraka iwezekanavyo. Dk. Mahenge alisema jeshi hilo limeaminiwa na Rais Magufuli na kupewa jukumu la kujenga msikiti huo.

"Nawashukuru jumuiya hii kuchangisha mchango huo, inaonyesha jinsi gani suala la imani linavyowagusa watu," alisema Dk. Mahenge.

Alisema bado wanaendelea na ujenzi, hivyo kwa yeyote mwenye kuguswa, bado nafasi ya kuchangia ipo.

Meja Jenerali Mbuge alisema pamoja na wao kujenga msikiti, lakini wanachangia Sh. milioni tano, ili ziweze kusaidia ujenzi.

Alisema wamefanya hivyo ili kumuunga mkono Rais Magufuli katika jambo la kiimani, ambalo amelianzisha.

Alisema ujenzi huo unatarajia kuchukua miezi mitatu kuwa umekamilika.

Alisema JKT itakuwa mstari wa mbele kuhakikisha msikiti huo unakamilika bila kuchelewa. Kwa upande wa Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mariadhiano, Alhadi Mussa Salum, alisema Rais Magufuli amefanya jambo la kiimani, hivyo wao wanamwombea aendelee kuwa na moyo huo.

Alisema ujenzi wa msikiti ni jambo zuri kwa sababu amethamini nafasi ya Mungu katika kujitoa kwenye mambo yake yanayotakiwa kufanywa.

Alisema watu wanapaswa kuiga mfano wa serikali hii katika utendaji wao kwa sababu wanakumbuka kutoa sadaka kwa kujenga nyumba za ibada.

Hivi karibuni Rais Magufuli alichangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa Chamwino ambao utajengwa na JKT.



Kinamama wachuuzi wa nyanya na viazi vitamu wakiwa wamepanga bidhaa zao chini jirani na vifaa vya kuhifadhia takataka nje ya soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za walaji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Viwanda vya nondo vyapewa angalizo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

BARAZA la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeviagiza viwanda vya kuzalisha nondo na chuma nchini kuzingatia sera ya mazingira ya mwaka 1997, inayozuia matumizi ya kuni kwenye viwanda vyao.

Lengo la agizo hilo ni kutunza mazingira, vinginevyo vitachukuliwa hatua za kisheria.

Agizo hilo lilitolewa na kaimu Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Novatus Mushi, wakati akizungumza na Nipashe, kuhusu matumizi ya nishati mbadala kwenye viwanda vinavyozalisha nondo na chuma nchini ambavyo baadhi yao vinaendelea kutumia kuni na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mushi alisema walishapiga marufuku matumizi ya kuni kwenye viwanda hivyo ambavyo vina matumizi makubwa ya kuni, hivyo kukata miti mingi kwa ajili ya kuwashia matanuru ya kuyeyushia vyuma viwandani kwao.

"Agizo hili siyo jipya kwani ni sera ya kutunza mazingira tangu mwaka 1997, lakini bado kuna baadhi ya viwanda vinaendelea kupuuza sheria hiyo na kuendelea na matumizi ya kuni kwenye viwanda vyao," alisema.

Alifafanua kuwa hawatasita kuvichukulia hatua za kisheria ikiwamo kuvifungia uzalishaji nchini," alisema Mushi.

Alisema kutokana na uzalishaji wa nondo na vyuma kuhitaji joto jingi wazalishaji wa bidhaa hizo, wamekuwa wakikata miti kwa wingi maeneo ambayo siyo ya hifadhi na kusababisha jangwa katika maeneo husika na wakati sheria imeshazuia.

Alisema baada ya kutungwa kwa sheria ya mazingira, serikali iliingia ubia na wazalishaji wa nishati mbadala ambazo hazina madhara kwenye mazingira ili zianze kutumika kama chanzo cha nishati kwenye viwanda hivyo.

Aliongeza kusema viwanda hivyo vinatakiwa kutumia nishati mbadala wa kuni ambazo haziharibu mazingira kama vile mkaa mbadala, mkaa mweupe, gesi na makaa ya mawe.

Hivi karibuni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, aliiagiza NEMC kufanya msako na kuvichukulia hatua za kisheria viwanda vyote vya nondo na chuma vinavyotumia kuni kwenye shughuli zao.

Alisema agizo hilo ni kwa nchi nzima ili kunusuru mazingira ambayo yanaharibiwa kutokana na kukata miti inayotumika kwenye kuyeyushia nondo na vyuma hivyo na badala yake watumie nishati mbadala.

# Wakulima wa zabibu waomba kupewa bima

**Na Ibrahim Joseph**, DODOMA

WAKULIMA wa zao la zabibu mkoani Dodoma, wameiomba serikali na taasisi za kifedha zinazotoa huduma za bima kuwasaidia kuwakatia bima ili kuwalinda wakati wa majanga.

Hayo yalibainishwa na baadhi ya wakulima wa Kijiji cha Matumbulu kilichopo nje kidogo Jiji la Dodoma walipozungumza na Nipashe kuhusu hali ya kilimo cha zabibu.

Mmoja wa wakulima hao, Daniel Ngoima, aliomba serikali na taasisi zingine za kifedha kuwasaidia kuwakatia bima ili ziwasaidie wakati wa majanga.

Ngoima alitaja sababu ya kuhitaji bima za kilimo ni kutokana na wakulima wengi wa zao la zabibu kukosa mazao kwenye msimu huu kwa sababu ya mvua kubwa.

"Sisi wakulima hatuna bima ya kilimo cha zabibu, likitokea janga kubwa la mwaka huu la kunyesha mvua kubwa tunakosa mazao kwenye mashamba yetu," alisema.

Alibainisha kuwa zabibu ni zao ambalo halihitaji maji mengi, hivyo ikitokea mvua zikizidi kama msimu huu inakuwa ni changamoto kwao kupata mazao ya kutosha.

Alisema katika msimu wa kilimo mwaka huu wengi wemekosa mazoa kutokana na mvua nyingi zilizonyesha na kusababisha kuvuna kidogo.

Kadhalika, alisema katika msimu huu wapo ambao hawakuvuna kabisa na kusababisha kuyumba kwenye maisha kutokana na kutegemea fedha za zao hilo.

Aidha, alisema kama taasisi za kifedha zitajitokeza kuwasaidia bima, itawaokoa na hasara wakati wa majanga kama hayo yakijitokeza.

Kwa upande wake Victoria Zablon, alisema kilimo cha zabibu hakihitaji maji mengi na ndio maana katika msimu wa mvua mavuno yanakuwa kidogo.

Zablon alisema kilimo cha zabibu ya Dodoma kina misimu miwili ya mavuno ambayo ni msimu wa mvua na kiangazi na alibainisha kuwa msimu bora kwa wakulima ni kingazi kwa sababu hakuna mvua.

Kuhusu soko, alisema katika msimu huu wakulima waliofanikiwa kupata mazao ya zabibu wamepata bei nzuri kutokana na kampuni zinazonunua kuwafikia huko huko mashambani.

"Hakuna kitu ambacho kilikuwa kinatusumbua wakulima kama kutokuwa na uhakika wa soko hilo, lilikuwa linatukatisha tamaa, lakini mwaka huu waliofanikiwa wamepata fedha," alisema.

Alitaja bei ya zao hilo katika msimu huu kuwa ni kuanzia Sh. 1,500 hadi Sh. 2,000 kwa kilo na mkulima hatumii gharama za kusogeza barabarani kwa sababu wanunuzi wanafika kununua sham-





## DC ahamasisha ujenzi zahanati

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amewahimiza wananchi wilayani hapa kuendelea kujitoa kwa hali na mali kwenye ujenzi wa zahanati na vituo vya afya badala ya kuendelea kuisubiri serikali.

Mfune alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na Nipashe juu ya upatikanaji wa huduma za afya wilayani hapa ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015.

Alisema ilani ya CCM imeweka wazi ushiriki wa wananchi katika kuchangia ujenzi wa huduma za afya na kwamba serikali itahakikisha ikamilishe ujenzi pamoja na kupeleka vifaa tiba na wataalamu.

Kwa mujibu wa Mfune, mwitikio wa wananchi hauridhirishi katika kujitoa kujenga vituo vya afya na zahanati huku wakitegea wakiisubiri serikali kuwajengea, jambo ambalo linawachelewesha kupata huduma za matibabu.

"Uhitaji wa huduma za afya ni mkubwa katika jamii zetu. Nawaomba wana-Mbarali tuendelee kujitoa kujenga tusiisubiri serikali acha itukute tunaendelea maana hapa tunajikomoa wenyewe," alisema Mfune.

Aliongeza kuwa serikali kwa kuwajali wananchi wake, imekamilisha ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya ambayo tayari imeanza kufanya kazi.

Mbali na jitihada za kuboresha huduma za afya, alisema serikali pia imekuwa ikiwasaidia wazee kwa kuhakikisha wanapata matibabu kwenye mazingira rafiki.

Alidai, alisema serikali imekuwa ikitoa gawio la fedha kupitia mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kujikimu na kwamba baadhi ya wazee wanatumia fedha hizo kuanzisha miradi ikiwamo ufugaji na wengine wanazitumia kusomesha watoto.

Katibu wa Baraza la Wazee wilayani hapa, Hezron Kapwela alisema maeneo mengi hayana vituo vya afya na zahanati hali inayosababisha wazee kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

# Msimamizi aonya chuki, matusi mikutano ya kampeni uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MSIMAMIZI wa Uchaguzi katika Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Kivuma Msangi, amewaomba wagombea wote kuhakikisha wafanya kampeni za kistaarabu ili kuepuka migogoro na uvunjifu wa amani.

Msangi alisema hayo juzi wakati akitaja majina ya watu walioteuliwa kugombea nafasi hizo baada ya kukidhi matakwa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Alisema kipindi cha kampeni kinahitaji ustaarabu kwa kila chama kwa kuhakikisha wanazingatia kanuni na sheria wanapokuwa majukwaani wakati wa kunadi sera zao.

"Ninawaomba wagombea wa kuzingatia maelekezo ya NEC. Hatuhitaji kupanda chuki wala kutengeneza uadui katika kipindi hiki. Kila mmoja aheshimu chama cha mwenzake, tunahitaji kampeni safi na uchaguzi wa amani," alisema Kivuma.

Pia aliwaomba wagombea wote kutumia lugha za staha wanapokuwa majukwaani ili kutoumiza kundi au chama fulani.

Alisema akiwa msimamizi wa uchaguzi, hatafurahishwa kuona wagombea wanakuwa sehemu ya kuhamasisha vurugu na chuki zinazoweza kuwa chanzo cha kuvunja amani.

Naye mgombea ubunge wa Jimbo la Mbarali kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Francis Mtega, alisema kwa kushirikiana na chama chake atahakikisha anasimamia kikamilifu amani na mshikamano katika kipindi chote cha kampeni.

"Nakishukuru sana chama changu kuniamini na kunipa ridhaa ya kupeperusha bendera. Nitahakikisha nafuata maelekezo yote ninayopatiwa," alisema Mtega.



Mgombea ubunge kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya, Francis Mtega (aliyevaa kofia nyeusi) akicheza muziki na viongozi wengine wa chama hicho, baada ya kurejesha fomu kwenye ofisi za msimamizi wa uchaguzi jimboni humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TARI yaelekeza nguvu kilimo hifadhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KUTOKANA na mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu wa mazingira nchini, watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Uyole mkoani Mbeya, wamesambaza teknolojia ya kilimo hifadhi, ili kuwasaidia walioathiriwa na kuongeza uzalishaji wa chakula. Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la shamba darasa lililoko kwenye Viwanja vya Maonyesho ya Kilimo vya John Mwakangale.

Alisema wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Rukwa, Iringa, Mbeya, Njombe na Katavi, wameshaanza kuona mafanikio kutokana na kutumia uhifadhi wa rasilimali udongo na mazingira katika maeneo yao.

Aliongeza kuwa kilimo hicho kinafuata kanuni kwa kulima kilimo cha mzunguko cha mazao ya nafaka na mikunde ambayo yamekuwa yakiongeza mbolea na uhifadhi wa udongo katika shamba.

"TARI - Uyole imeamua kuhimiza kilimo hifadhi kwa sababu kinaongeza uzalishaji kwenye maeneo yenye ukame. Pia kinawahakikishia wakulima usalama wa chakula pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji, hivyo kuongeza kipato kwa mkulima," alisema Dk. Bucheyeki.

Aliongeza kuwa kilimo hifadhi pia kinasaidia kupunguza muda wa kufanya kazi shambani, hivyo mkulima anapata muda wa kufanya shughuli zingine za maendeleo pamoja na kudhibiti mmomonyoko wa udongo na kumudu mabadiliko ya tabia nchi.

Sambamba na hilo, alisema kilimo hifadhi kinakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa wataalamu wenye elimu ya kilimo hifadhi, huku akieleza bado eneo linalolimwa kwa kilimo hicho ni dogo ambapo mpaka mwaka 2012 ni ekari 62,500 tuu ndizo zilitumia teknolojia hiyo.

Alisema TARI imejipanga kuhakikisha teknolojia zinazozalishwa zinasambazwa na kuwafikia wakulima na wadau wengine wa kilimo ili kuweza kuongeza uzalishaji wa malighafi za zinazotokana na kilimo zinazohitajika katika uchumi wa viwanda.



# Wananchi waaswa matumizi ya barabara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wakati Serikali ya Zanzibar ikiendeleza kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya barabara kwa kutumia gharama kubwa, wananchi wana wajibu wa kuzingatia matumizi bora ya rasilmali hiyo muhimu katika mwenendo wa uchumi wa Taifa.

Balozi Iddi alisema hayo alipofanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara nne zinazojengwa katika kiwango cha lami chini ya usimamizi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar na Benki ya Kiarabu inayosimamia Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika (BADEA). Barabara hizo ni pamoja na iliyoanzia Kinduni hadi Kitope yenye urefu wa kilomita nne, Mwera Mambo hadi Mashine ya Maji Meli Tano ikiwa na urefu wa kilomita 3.4, Fuoni Polisi hadi Kibonde Mzungu Daraja la Dk. Shein kilomita 1.2 na inayoanzia Mtaa wa Jumbi hadi Koani kilomita 6.3.

Balozi Iddi alielezea kuridhishwa na kazi kubwa inayofanywa na wahandisi wazalendo katika kuweka miundombinu safi na imara ya barabara jambo ambalo litaleta faraja kubwa kwake na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, watakapopumzika baada ya utumishi wao kwa umma.

Balozi Iddi aliwashauri wahandisi hao wakati wanapokabidhiwa jukumu la kuimarisha miundombinu wakazingatia vyema mbinu na mikakati ya kisasa kutokana na uhaba wa rasilimali ya mchanga unaovikabili Visiwa vya Zanzibar hivi sasa. "Wahandisi na wananchi lazima waelewe kwamba Zanzibar kwa sasa ina upungufu mkubwa wa mchanga, hivyo katika miradi wanayoianzisha ni vyema wakazingatia changamoto hiyo ili wasikwame katika kazi yao," alisema Balozi Iddi.

Aliishauri wizara inayosimamia masuala ya ujenzi pamoja na ya fedha kuhakikisha kwamba suala la malipo linafanyika kabla ya kukabidhiwa miradi husika, na haitopendeleza kuona mradi unamalizika na kukabidhiwa ukiwa na deni.

Aidha, aliwataka vijana wanaoendesha vyombo vya moto kwa mwendo wa kasi kuacha mara moja tabia hiyo kwa vile wagharimu maisha ya wananchi hususan wazee na watoto.

Alisema uimarishaji wa miundombinu unaofanywa na serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo unazingatia kuwarahisishia wananchi usafiri katika harakati zao za kujitafutia riziki.

Wakitoa ufafanuzi wa kazi zinazoendelea za ujenzi wa miundombinu hiyo, wahandisi wasimamizi wa miradi hiyo walisema yapo matumaini makubwa ya miradi hiyo kukamilika katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa mikataba yake.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, waliipongeza na kuishukuru serikali kwa umakini wake wa kupambana na changamoto zinazowakabili wananchi.




Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu ya uteuzi wa mgombea wa nafasi hiyo, katika Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), eneo la Maisara, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZHELB yasitisha mikopo kwa watumishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BODI ya Mikopo Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB), imezuia utoaji wa mikopo kwa wafanyakazi wote wa serikali ili kutoa fursa kwa vijana wasiokuwa na ajira kupata mikopo.

Bodi hiyo imesema utaratibu huo umeanza mwaka huu kwa lengo la kutoa fursa kwa wanafunzi waliofaulu vizuri mwaka huu kupata mkopo.

Mkurugenzi wa bodi hiyo, Iddi Haji Khamis, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana Mjini Zanzibar.

Alisema, serikali imeanza utaratibu huo kuhakikisha watumishi wote wa serikali wanasomeshwa na wizara inayohusika na utumishi wa umma.

Alisema idadi ya wanafunzi imekuwa ikiongezeka kila mwaka na vijana wanaomaliza stashahada, hivyo hatua hiyo itasaidia fedha hizo kubakia na kutumika kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu.

"Hii kwetu ni faraja kuona nafasi 1,600 ambazo zilikuwa zikipatikana zitaongezeka na vijana wetu wengi wataweza kujiunga na elimu ya juu," alisema. Hata hivyo, alisema pamoja na kuongeza nafasi kwa mfumo huo, pia bodi hiyo imetakiwa kupunguza upelekaji wanafunzi nje ya nchi kwa fani ambazo zinapatikana Tanzania.

Alisema Tanzania ina zaidi ya vyuo vikuu vya elimu ya juu 60 na vitatoa wataalamu wa fani mbalimbali.

"Mwaka jana tulikuwa na wanafunzi wa vyuo vya nje zaidi ya 400 na pesa wanazozitumia ni nyingi ukilinganisha na wale wanaosoma vyuo vya ndani ya nchi yetu, ikiwamo kulipia ada, posho na mambo mengine," alisema.

Alisema bodi itatoa mkazo kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya ndani, hivyo aliwasisitiza wanafunzi kuhakikisha wanajiunga na vyuo vya ndani ili kuepusha gharama ambazo zisizokuwa za lazima.

Alisema bodi hizo zinashirikiana pamoja ili kuona wananchi hasa vijana wanafaidika na bodi hizo.

Hata hivyo, alisema tayari bodi zimeshaanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na elimu ya juu hivyo ni vyema wanafunzi kutumia fursa hiyo.

# Anayeshtakiwa kuchoma sindano watoto akiri kosa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MSHTAKIWA Salum Ali Malik (26), mkazi wa Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja, anayekabiliwa na shtaka la kuwachoma watoto sita sindano inayodaiwa kuwa ya sumu, amekubali makosa yake mbele ya Mahakama ya Mwanzo Mwanakwerekwe.

Kesi hiyo ambayo ilifunguliwa mahakamani hapo Agosti 10, mwaka huu ambapo mshtakiwa huyo alisomewa shtaka hilo kwa mara ya kwanza, lakini alikana.

Hata hivyo, Agosti 24, mwaka huu kesi yake ilipofikishwa tena kwa ajili ya kusikilizwa, alikiri kutenda kosa hilo. Hakimu wa Mahakama ya Mwanakwerekwe, Mohammed Ali Kombo, alimtia hatiani mshtakiwa huyo na kumtaka kulipa faini ya shilingi 50,000 kwa kila kosa na kulipa fidia ya shilingi 100,000 kwa kila mwathirika na akishindwa atatumikia kifungo cha mwezi mmoja jela.

Mahakama hiyo ilimtaka mshtakiwa huyo kutumikia adhabu hizo tofauti. Hata hivyo, alilipa faini hiyo.

Naye Mwendesha Mashtaka, Koplo Vuai Ali Vuai, alidai kuwa mshtakiwa huyo alipatikana na makosa sita ya shambulio la kawaida kinyume cha kifungu cha 229 cha sheria ya makosa ya jinai namba 6 ya mwaka 2018 sheria za Zanzibar.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo Januari 10, mwaka huu, saa 10:00 jioni huko Kwamtipura Wilaya ya Mjini Unguja, bila ya halali alimshambulia Hafidh Rashid Omar (4) kwa kumchoma sindano katika kidole cha mkono wake wa kulia na kumsababishia kupata maumivu makali mwili mwake.

Aidha, alidai mshtakiwa huyo siku hiyo hiyo katika maeneo hayo alimshambulia mtoto Mudrik Muridu Azan (5), kitendo ambacho ni kosa kisheria.

Katika kosa jingine, mshtakiwa huyo alidaiwa kumchoma sindano katika kiwiko cha mkono wake wa kulia Abdullatif Rashid Omar (14).

Kadhalika, mshtakiwa huyo alidaiwa kumshambulia kwa kumbinya mkono wake wa kulia na kumchoma sindano Nurdin Seif Hamad (5) na kumsababishia maumivu mwilini mwake.

Pia ilidaiwa kuwa siku hiyo hiyo mshtakiwa huyo alimshambulia Ali Said Ali (4) kwa kumchoma sindano kidole chake cha gumba cha mkono wa kushoto na kumshambulia Yussuf Juma Makame (4) kwa kumbinya mkono wake wa kulia kisha kumchoma sindano na kumsababishia kupata maumivu makali.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wazazi wa watoto hao walisema kuwa hawajaridhika na hukumu ya mahakama.

Rashid Omar, mzazi wa watoto wawili kati ya sita waliojeruhiwa na mshtakiwa huyo, alisema kuwa adhabu iliyotolewa ni ndogo kulingana na kosa hilo ambalo linahatarisha uhai wa watoto hao.

Alisema kwa kuwa keshi hiyo ni ya Jamuhuri, aliiomba Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kukata rufani ili haki iweze kutendeka.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi kwa na biashara. **Mawasiliano: 0757 079057.**

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**GENERATE MONEY AND JOBS**

- Learn Designing winning Project Proposals
- Access Donors.
- Establish NGO
- **0784 505108/0718 437371/ 0769 505108**


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### TAARIFA KWA UMMA



**LAYLA RAHIB MSUYA** amepote tangu tarehe 04/07/2020 huko **Mtipa Singida .**

Yeyote atakaemuona atoe taarifa kw **No: 0718 960256, 0785 298157 na 0784 243841** au atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu naye.

Taarifa Polisi: **SDG/RB/4428/2020**

115873302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;244/2020**

**Ombi la ZAWADI SAID MWINYIMBEGU,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAID MWINYIMBEGU.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 26/08/2020.

Sahihi ya Hakimu

115874402

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JUMA MOURICE KAMANGA** amepotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 224 BZK na MC 608 CAH.** Aina zake **HAOJUE.**

Yeyote atakae ziona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa ya polisi :

**MOR/MOR/RB/617390/2020.**

115874502

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**PENDAEL JONATHAN MANUMPA.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya shineray yenye usajili na. **T 976 BXA.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**DOM/KIB/RB/605451/2020**

115874302

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MILTON BLASTO MAKUNDI** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 973 CDJ** aina yake **SUZUKI JIMMY.** Yenye chassis namba **JB33W107479** na Engine namba **913B607420**

Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**DSM/PHQ/RB/587478/2020.**

115874202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO- MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI 334 na 335 ZA 2020**

**MDAI...............WANTORA J.N. BUSINESS SOLUTION CO.LTD**

**DHIDI YA**

**WADAIWA............................. 1.AMIRI HAJI SAID na**
**2. MICHAEL MAKARIOS NGONYANI**

Kwa kuwa mdai tajwa hapo juu alifungua mashauri dhidi yenu wadaiwa tajwa hapo juu.
Mnaamriwa na Jamhuri kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 01/09/2020 bila kukosa ili kuja kujibu madai hayo dhidi yenu.
Endapo hamtahudhuria mbele ya Mahakama siku hiyo shauri/mashauri hayo yatasikilizwa upande mmoja(Exparte Hearing) na kutolewa maamuzi.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21/08/2020.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI
DODOMA

115873102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo ya DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 91/ 2020.**

**Ombi la MUSA MAKONGORO SABBY kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu DEBORA MRAMBA MRAMBA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 31/08/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 13/08/2020.

115874102

---

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**TMC/LD/MKJ/12506**

**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: ANEU ABIUDI SALEMA**

**ARDHI: KIWANJA NA. 991/189 KITALU C ENEO LA MTONI KIJICHI MANISPAA YA TEMEKE JIJINI DAR ES SALAAM**

Taarifa inatolewa kwamba BARUA YA **TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** ilitajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja tangu tarehe ya taariffa hii ilipotangazwa katika gazeti.

**BARUA HALISI YA TOLEO** ikipatikana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE S.L.P 46343 DAR ES SALAAM.**

P. A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

115873202

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MATHIAS ALISEN KISUKARI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COSTA** yenye namba ya usajili **T371 ASF** iliyotolewa na mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:

**DAR/KJN/RB/948/2020**

115872502

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RICHARD SWETALA MWAKYONDE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba ya usajili **T855 DMB** iliyotolewa na mamlaka ya mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:

**DAR/KJN/RB/621130/2020**

115873702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO- MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI 334 na 335 ZA 2020**

**MDAI...............WANTORA J.N. BUSINESS SOLUTION CO.LTD**

**DHIDI YA**

**WADAIWA............................. 1. PHILIAS RICHARD MBUYA na**
**2. HASSAN JAKU HASSAN**

Kwa kuwa mdai tajwa hapo juu alifungua mashauri dhidi yenu wadaiwa tajwa hapo juu.
Mnaamriwa na Jamhuri kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 28/08/2020 bila kukosa ili kuja kujibu madai hayo dhidi yenu.
Endapo hamtahudhuria mbele ya Mahakama siku hiyo shauri/mashauri hayo yatasikilizwa upande mmoja(Exparte Hearing) na kutolewa maamuzi.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 17/08/2020.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI
DODOMA

115873102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA RUNGWE**

**LILILOPO TUKUYU**

**KESI NA.15/2019**

**EVANCE ALIFA MARCO................................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**RICHARD MWAMBUSI...........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: RICHARD MWASUMBI**
Muombaji aliyetajwa hapo juu,amefungua kesi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumbala wilaya ya Rungwe.Unaarifiwa kufka Baraza la Ardhi na Nyumba tarehe 28/08/2020 ,saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Usipofika kama ulivyoamriwa,shauri hili litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.
Unatakiwa kufika bila kukosa wewe au wakili wako au mtu yeyote utakayempa maelezo kamili.
AMRI hii imetolewa na mkono wangu na muhuri/lakiri ya baraza hili tarehe 21/08/2020.

T. MUNZERERE
MWENYEKITI WA BARAZA

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEX R. NTANGULIGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **TOYOTA HARRIER** yenye namba za usajili **T774 CGS** Chassis no. **SXU10-0034215,** Engine no. **5S129883.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**OB/RB/10732/2017**

115870002

---


**Uza,**

**Chenye Thamani**

**Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati ya na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Mazungumzo hatima Mali yakwama

**BAMAKO,** Mali

**Keita amekaririwa akisema kuwa alijiuzulu kwa hiyari na sasa anataka kuona taifa hilo linapata serikali ya mpito itakayorejesha utawala wa kidemokrasia.**

MAZUNGUMZO kati ya wawakilishi wa mataifa ya Afrika Magharibi na viongozi wa Jeshi la Mali, yameshindwa kufikia makubaliano ya namna ya kurejesha utawala wa kiraia nchini humo, baada ya mapinduzi ya wiki iliyopita.

Mkwamo katika suala la kuirejesha Mali chini ya utawala wa kiraia, umeibuka baada ya majenerali wa jeshi kukataa pendekezo hilo na kutaka kupewa miaka mitatu ya kipindi cha mpito kitakachoongozwa na mwanajeshi.

Msemaji wa kundi la wanajeshi walioongooza mapinduzi, Kanali Ismael Wague, alisema licha ya majadiliano yanayoendelea mpango wa mwisho wa kipindi cha mpito nchini Mali utaamuliwa na makamanda wa jeshi, baada ya mashauriano mapana na makundi mengine ya kiraia.

Msimamo huo wa Baraza la Kijeshi wa kuitisha uchaguzi baada ya miaka mitatu ulitolewa kwa mara ya kwanza siku ya Jumapili, lakini tangu wakati huo umekabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa raia wa Mali na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS).

ECOWAS -- Jumuiya inayounda na mataifa 15 -- ilituma ujumbe wa ngazi ya juu mjini Bamako siku ya Jumamosi, kuhimiza matakwa yake ya kurejea kwa utawala wa kiraia nchini Mali.

Mkuu wa Ujumbe wa ECOWAS ambaye pia ni Rais wa zamani wa Nigeria, Goodluck Jonathan, alisema wamefanikiwa kupata makubaliano katika baadhi ya masuala muhimu, lakini wamepeana muda wa kuyatafakari mengine ambayo hawakufikia mwafaka.

Zaidi kuhusu msimamo wa ECOWAS kuelekea hatma ya utawala nchini Mali, Jonathan alisema: "ECOWAS hatutokuja na kuwawekea serikali watu wa Mali, iwe serikali ya kuchaguliwa au serikali ya kuteuliwa ya kipindi cha mpito ni lazima iamuliwe na watu wa Mali"

Hayo yanajiri wakati duru zimearifu Rais aliyepinduliwa Ibrahim Boubacar Keita, ambaye ECOWAS ilishinikiza kurejeshwa madarakani amearifu kuwa hana nia ya kuendelea tena kuongoza nchi hiyo. Keita amekaririwa akisema kuwa alijiuzulu kwa hiyari na sasa anataka kuona taifa hilo linapata serikali ya mpito itakayorejesha utawala wa kidemokrasia.

Kundi la wanajeshi lililompindua Keita Agosti 18, liliahidi siku moja baada ya mapinduzi kuwa litaunda kipindi cha mpito kitakachoongozwa na raia na kuitisha uchaguzi mkuu katika muda mfupi unaokuja.

Viongozi wakuu wa ECOWAS wanatarajiwa kuwa na mkutano wa pamoja siku ya Jumatano kuamua namna ya kushughulikia mzozo wa Mali, wakikubaliana namna mapinduzi ya mwisho nchini humo mwaka 2012 yalivyoitikisa kanda hiyo na kuchochea kuibuka kwa uasi wa makundi ya itikadi kali.

ECOWAS tayari imetishia kuiwekea vikwazo Mali iwapo ufumbuzi hautapatikana kuhusu nani ataongoza nchi hiyo wakati wa kipindi cha mpito na lini hasa uchaguzi mkuu utaitishwa kurejesha utawala wa kiraia. **DW**



Mazungumzo yakiendelea kati ya viongozi wa jeshi la Mali na ujumbe wa ECOWAS. **PICHA: REUTERS**

## UN 'yapiga chini' ombi la Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) limeyapinga matakwa ya Marekani kurejesha vikwazo vyote dhidi ya Iran, huku mjumbe maalum wa Marekani katika umoja huo, akiwashutumu waliopinga kwa kuunga mkono magaidi.

Balozi wa Indonesia UN ambaye kwa sasa ndiye rais wa kupokezana wa Baraza la Usalama, Dian Triansyah Djani, alitoa tangazo hilo kufuatia maombi ya Urusi na China kutaka matokeo ya kura ya maoni ya wanachama wote 15 wa baraza hilo kuhusu ombi la Marekani yatangazwe.

Wiki iliyopita, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alisisitiza kuwa Marekani ina haki kisheria kuvirudisha vikwazo vya UN dhidi ya Iran, licha kuwa Rais Donald Trump alishaiondoa nchi yake kwenye mkataba wa nyuklia wa mwaka 2015, kati ya Iran na nchi nyingine sita zenye nguvu kubwa ulimwenguni, ambao uliidhinishwa na Baraza la Usalama la UN.

Wanachama wote isipokuwa Jamhuri ya Dominika, walimwambia rais wa baraza hilo kwamba, hatua za utawala wa Marekani ni kinyume cha sheria kwa sababu mwaka 2018 Rais Trump alijiondoa kwenye mkataba huo uitwao kwa kifupi JCPOA.

Djani aliwaambia wanachama wa Baraza wakati wa mkutano kwa njia ya video kwamba hakuna makubaliano ya pamoja kuhusu suala hilo. **DW**

## 'Aliyepigwa risasi Marekani anahitaji miujiza kutembea'

**WASHINGTON,** Marekani

MAWAKILI wa familia ya mtu mweusi aliyepigwa risasi na polisi katika jimbo la Wisconsin nchini Marekani wamesema anahitaji miujiza kutembea tena.

Jacob Blake (29), alipigwa risasi mara kadhaa akifungua mlango wa gari mjini Kenosha.

Mawakili hao walisema moja ya risasi alizopigwa ilipitia katika uti wake wa mgongo kwamba kumetibua maandamano na ghasia.

Gavana wa Wisconsin ametuma wanajeshi zaidi wa ulinzi wa kitaifa Kenosha.

Taarifa zaidi zinadai kuwa Blake kwa sasa amepooza, na madaktari hawana hakika ikiwa atafanikiwa tena kutumia miguu yake

"Familia yake inaamini miujiza inaweza kutokea, lakini matokeo ya uchunguzi wa kimatibabu yanaonesha kwa sasa amepooza, kwa sababu risasi hizo zilijeruhi uti wake wa mgongo, itakuwa miujiza kwa Jacob Blake Jr kutembea tena," wakili Ben Crump aliwaambia wanahabari.

Blake, alipigwa risasi mbele ya watu waliokua ndani ya gari, aliachwa na mashimo ya risasi tumboni, kujeruhiwa mkono pamoja na figo na ini lake.

Sehemu kubwa ya utumbo wake ulitolewa, mawakili wake waliwambia wanahabari.

Mama yake Julia Jackson aliwafahamisha wanahabari kwamba mwanawe anapigania maisha yake, lakini angelijua kinachoendelea kwa sasa, maandamano na uharibifu, asingefurahi hata kidogo.

Picha kutoka mji huo uliopo kilo mita 100,000 kusini magharibi mwa ziwa Michigan, zinaonesha majengo na magari yalioharibiwa kufuatia maandamano ya siku mbili nyakati za usiku kupinga ukatili wa polisi.

Siku ya Jumanne, Gavana Tony Evers alisema atawapeleka walinzi zaidi wa kitaifa mjini Kenosha kuchunguza majengo ya serikali na kuwapa ulinzi wazima moto. Hali ya hatari pia imetangazwa Wisconsin.

Tukio la kupigwa risasi kwa Blake limetokea wakati ambao Idara ya polisi nchini Marekani inakabiliwa na tuhuma za kuwanyanyasa Wamarekani weusi, huku suala la ubaguzi wa rangi likiendelea kuwa chanzo cha mgogoro katika jamii, tangu kutokea kwa kifo cha raia mwingine mweusi mikononi mwa polisi mjini Minneapolis, George Floyd, Mei, mwaka huu. **BBC**

## HABARI MICHEZO



# KLOPP HANA HOFU MAJERUHI YA VAN DIJK

**VIENNA,** Austria

KOHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesisitiza majeruhi aliyoyapata Virgil van Dijk Jumanne kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Salzburg si kitu cha kukifikiria sana.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alilazimika kutolewa nje katika dakika ya 55 kwenye mchezo huo wa sare ya kufungana mabao 2-2 nchini Austria baada ya kuchanika sehemu ya kichwa chake. Hata hivyo, Klopp alithibitisha baada ya mchezo huo kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, hakuumia sana.

"Virg aliwekwa tu plasta, hajaumia sana, alichanika kidogo kichwani," alisema Klopp akinukuliwa na tovuti ya Klabu ya Liverpool.

"Si tatizo. Kwa wakati huu anaendelea vizuri si majeraha ya kuyafikiria sana kwa sasa."

Liverpool itacheza na Arsenal kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii Jumamosi kabla ya kuanza kwa Ligi Kuu ya England dhidi ya Leeds United, Septemba 12.



# Leeds yaipiku Barca, Atletico kwa Moreno

**VALENCI,** Hispania

LEEDS United imefikia makubaliano na Valencia kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji nyota, Rodrigo Moreno, klabu hiyo ya LaLiga imethibitisha.

Valencia ilitangaza Jumanne kwamba, ilikuwa kwenye mazungumzo ya awali na Leeds juu ya usajili wa Rodrigo, lakini sasa klabu hiyo iliyopanda Ligi Kuu ya England imemtia mikononi mwake.

Rodrigo alikuwa akihusishwa sana na miamba wa LaLiga, Barcelona na Atletico Madrid, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania ameamua kujiunga na Leeds kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 30.

"Valencia CF imefikia makubaliano na Leeds United FC Jumanne hii kwa ajili ya usajili wa Rodrigo Moreno," ilisema taarifa ya Valencia.

"Valencia CF inapenda kumshukuru kwa kipindi chote ambacho amecheza hapa ambapo amecheza jumla ya mechi 220 na kufunga mabao 59. Tunamtakia kila la heri."

Rodrigo ambaye alijiunga na Valencia kwa mkataba wa moja kwa moja mwaka 2015 baada ya awali kutua kwa mkopo akitokea Benfica msimu wa 2014/15, ni mchezaji wa kwanza mkubwa kuondoka pale Mestalla.

# Conte bado yupo sana ukocha Inter Milan

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte atabakia kama kocha mkuu wa Inter, klabu hiyo ya Serie A, imethibitisha.

Kocha huyo wa zamani wa Juventus na Italia, alizungumzia majaliwa yake Ijumaa iliyopita baada ya Inter kufungwa kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Europa na Sevilla, akisema Inter lazima ipange maisha "na yeye au bila yeye."

Conte alisema kwamba "kitu fulani kilitokea" na pia alidokeza kuhusu majukumu ya kifamilia, akihoji kama soka linatakiwa kuwa kipaumbele chake.

Inter ilimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Serie A, na kutinga nusu fainali ya Coppa Italia.

Conte sasa atakuwa na nafasi ya kukijenga upya kikosi hicho kwa ajili ya msimu unaokuja wa Ligi Kuu.

Taarifa ya klabu hiyo katika tovuti yake ilisomeka: "Klabu na Antonio Conte walikuwa na mkutano wenye mafanikio na pande zote mbili zimekubaliana kuendelea na mradi tulioanza wa kuijenga klabu hii."



## HABARI MICHEZO

# AJAX YAKATA TAMAA KUMREJESHA SUAREZ




**AMSTERDAM,** Uholanzi

MKURUGENZI wa soka wa Ajax, Marc Overmars, amesema nafasi ya klabu hiyo kumsajili tena nyota wa Barcelona, Luis Suarez ni "ndogo".

Suarez mwenye umri wa miaka 33, ameripotiwa kuambiwa kwamba hayupo kwenye mipango ya Barca na kocha mpya, Ronald Koeman, ambaye anajaribu kuijenga upya timu hiyo.

Ajax ilionekana kuwa na nafasi kubwa ya kumsajili Suarez, ambaye alitumia miaka minne akiwachezea mabingwa hao wa Eredivisie kabla ya kujiunga na Liverpool mwaka 2011.

Huku kukiwa na uvumi wa Ajax kuingia kwenye mazungumzo ya kutaka kumsajili Suarez na kutua pale Amsterdam, Overmars ameelezea uvumi huo.

"Ngoja niweke hivi: nafasi ya kumsajili ni ndogo," alisema Overmars akiiambia Ziggo Sport mara baada ya Ajax kuchapwa bao 1-0 na Hertha Berlin kwenye mchezo wa kirafiki Jumanne.

"Hilo ni jibu la wazi kabisa nafikiri. Haijalishi kama kumekuwa na mawasiliano na yeye. Kwani tumekuwa tukiwasiliana na wachezaji wetu wa zamani mara zote."

Suarez, ambaye alishinda taji la Eredivisie na KNVB wakati akicheza pale Ajax, amesherehekea mataji manne ya LaLiga na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipotua hapo mwaka 2014.

## Manchester, PSG ziulizwe kuhusu Koulibaly- Napoli

**NAPLES,** Italia

RAIS wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, amesema Manchester United, Manchester City au Paris Saint-Germain ndizo zinatakiwa kujibu swali kuhusu mlinzi, Kalidou Koulibaly.

Koulibaly amekuwa akihusishwa sana na kwenda City, huku wapinzani wao wa EPL, United na mabingwa wa Ligue 1, PSG wamekuwa wakihusishwa pia na kumuwania.

Majaliwa ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal yametawala vyombo vya habari, huku Napoli ikiripotiwa kutaka kutafuta fedha ili kumsajili mlinzi Gabriel Magalhaes kutoka Lille, licha ya Arsenal kuwa na nafasi kubwa zaidi.

Alipoulizwa kuhusu Koulibaly, De Laurentiis alijibu swali hilo kiaina yake.

"Unatakiwa kuwauliza Manchester United, City au PSG swali hilo," alisema. "Kwa maneno mengine, wote wenye uwezo wa kulipa kiasi kikubwa cha fedha."

Koulibaly amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa mabeki bora duniani tangu alipojiunga na Napoli akitokea Genk mwaka 2014.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, ameisaidia Napoli kushinda Kombe la Coppa Italia (2019-20) na Supercoppa Italia (2014).




# Maguire atemwa kikosi cha England



**LONDON,** England

NAHODHA wa Manchester United, Harry Maguire, ameondolewa katika kikosi cha England na kocha Gareth Southgate baada ya kupewa kifungo cha nje katika Kisiwa cha Ugiriki cha Syros.

Maguire mwenye umri wa miaka 27, alitajwa kwenye kikosi cha Southgate mapema juzi wakati kesi yake ikiendelea kabla ya kutolewa hukumu.

Southgate amesema uamuzi wa kumuondoa Maguire kwenye kikosi hicho ambacho kinajiandaa kwa mashindano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa mwezi ujao ni "muhimu kwa maslahi ya pande zote mbili".

Maguire alipatikana na hatia baada ya kujaribu kutoa rushwa kwa polisi akiwa katika mapumziko binafsi Kisiwani Syros na amehukumiwa kifungo cha nje cha miezi 21 na siku 10.

Mlinzi huyo raia wa England alianza kutuhumiwa wiki iliyopita kwa kosa na kujaribu kutoa rushwa, kutoleana maneno ya matusi na polisi akiwa Mykonos.

Maguire alisema Jumanne alimpa maelekezo yote mwanasheria wake kuhusiana na taratibu za mahakamani ya kule Ugiriki pamoja na mchakato wa kukata rufaa ya hukumu hiyo.

"Niko sawa, nina nguvu na naamini kuwa kila jambo hutokea kwa sababu, tuko sawa kifamilia na rafiki zangu," alisema Maguire.

Anawakilishwa na Alexis Anagnostakis, wakili maarufu anayetetea haki za binadamu huko Ugiriki ambaye alitaka kesi hiyo kuahirishwa, lakini ombi hilo likakataliwa.

Alikamatwa pamoja na kaka yake Joe mwenye umri wa miaka 28 na rafiki yake, Christopher Sharman mwenye umri wa miaka 29, siku ya Alhamis iliyopita baada ya kushindwa kuelewana na polisi.

Taarifa ya klabu Manchester United ilieleza: "Harry Maguire alisema hajahusika na makosa yote yaliyotajwa hapo juu, ameendelea kuwa imara sana.

"Na baada ya kukutwa na hatia hiyo Maguire, nahodha wetu ametuambia amepanga kukataa rufaa."

Polisi mmoja alidai kwamba akiwa kituoni, Maguire alimuuliza "unajua mimi ni nani? Ni nahodha wa timu ya Manchester United, Nitajiri sana, naweza kukupa fedha, naweza kuwalipa, tafadhali tuachieni tuondoke."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AOMBA RASMI KUTIMKA BARCELONA

●●● Amwambia Koeman alikuwa anajifunza namna ya kuondoka Camp Nou, Carles Puyol amsapoti...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi ameiambia Barcelona anataka kuondoka klabuni hapo wakati wa kipindi hiki cha majira ya joto.

**Nahodha huyo wa Barca, Messi ambaye mkataba wake unamalizika Juni 2021, amesema ana kipengele kwenye mkataba wake kinachomruhusu kuondoka akiwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu uliopita wa 2019-20.**

Kipengele hicho kilimalizika muda wake Mei mwaka huu, lakini kutokana na ligi kusogezwa mbele hadi Agosti baada ya mlipuko wa virusi vya corona, mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or amewaambia miamba hao wa Catalunya bado anataka kutumia kipengele hicho.

Messi wiki iliyopita alifanya mazungumzo na kocha mkuu mpya, Ronald Koeman, ambaye amechukua mikoba ya Quique Setien baada ya Barca kuchabangwa mabao 8-2 na Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, aliripotiwa kumuambia Koeman alikuwa anajifunza namna ya kuondoka hapo Camp Nou na Stats Perform News imethibitisha kwamba ameamua kutimiza azima yake hiyo baada ya rafiki yake wa karibu, Luis Suarez kuonekana hatakiwi tena kwenye klabu hiyo.

Huku pia nahodha wa zamani wa Barca, Carles Puyol, akionyesha kumuunga mkono kwa kuandika kwenye Twitter: "Heshima na kumpenda Leo. Nampa sapoti yangu yote, rafiki yangu."

Akiwa ametumia kipindi karibu chote cha uchezaji wa soka la kulipwa na Barca, Messi amekuwa akihusishwa na kurudi Argentina kucheza katika klabu yake ya utotoni ya Newell's Old Boys iliyopo mji wa nyumbani kwao, Rosario.

Pia kuna uwezekano wa kuungana na kocha wake wa zamani pale Barca, Pep Guardiola katika Klabu ya Manchester City, huku pia Inter Milan ikitajwa kumuwania.

Kwa mujibu wa TyC Sports, klabu za Ligi Kuu ya Marekani (MLS), nazo zinamtolea macho.

Messi mfungaji bora wa wakati wote wa Barcelona, ametikisa nyavu mara 634 na ametoa pasi za mwisho 276 katika mechi 731 alizocheza kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo.

Raia huyo wa Argentina alicheza mechi yake ya kwanza kwa kikosi cha kwanza cha Barcelona mwaka 2004 wakati akiwa na umri wa miaka 17 na ameshinda mataji 34 hapo Camp Nou.

## ZISIKUPITE

### PSG, UNITED ZAMTAKA MESSI

PARIS St-Germain na Manchester United zipo kwenye nafasi ya kumsajili Lionel Messi baada ya fowadi huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 33, kuiambia Barcelona anataka kuondoka - na zote zipo tayari kutoa ada. ***(Sport)***

### VARDY KUPEWA MKATABA

MSHAMBULIAJI wa Uingereza, Jamie Vardy mwenye umri wa miaka 33, atasaini mkataba mpya na Leicester. ***(Telegraph)***

### SILVA KUPIMWA CHELSEA LEO

THIAGO Silva mwenye umri wa miaka 35, anatarajia kufanyiwa vipimo vya afya pale Chelsea leo Alhamisi, licha ya Paris St-Germain kujaribu dakika za mwisho kumpa ofa ya mkataba mpya nyota huyo wa Brazil. ***(Sky Sports)***

### COUTINHO ATAKA KURUDI EPL

PHILIPPE Coutinho angependa kurudi Ligi Kuu ya England kuliko kubaki Barcelona - huku Manchester United, Arsenal na Chelsea zikionyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 28. ***(Marca)***

### ARSENAL KUMPOTEZEA PARTEY

ARSENAL inataka kuachana na dili la kumsajili kiungo wa Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 27, kutoka Atletico Madrid mwenye thamani ya pauni milioni 45. ***(Sport via Express)***

### YAMUWANIA RODRIGUEZ

EVERTON ipo kwenye mazungumzo ya kutaka kumsajili kiungo wa Real Madrid, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 29, huku kocha wake, Zinedine Zidane akiwa tayari kumuachia aondoke klabuni hapo. ***(Talksport)***

### NEWCASTLE YAMTAKA ROB

NEWCASTLE United inawania kumsajili kwa mkopo mlinzi wa kati wa Arsenal, Rob Holding mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

### AC MILAN YAMUWANIA DIAZ

AC Milan inapambana kumtaka kumsajili kwa mkopo kiungo wa Hispania, Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 21 kutoka Real Madrid. ***(Marca)***

### CRYSTAL YAMNYAKUA EZE

KLABU ya Crystal Palace imekubali ada ya pauni milioni 14 kwa kiungo wa QPR, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun)***

### YAJITOSA KWA WATKINS

FULHAM imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili fowadi wa Brentford, Ollie Watkins, mwenye umri wa miaka 24, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England nazo zikionesha nia. ***(Sky Sports)***

### NEILSON AGOMBEWA EPL

KLABU za Everton, Leicester City, Southampton na Leeds United zote zimetuma maskauti wao kwenda kumuangalia mlinzi wa kati wa Dundee United, Lewis Neilson mwenye umri wa miaka 17 raia wa Scotland. ***(Dundee Courier)***

HABARI MICHEZO

## Miembeni, Kikwajuni zashuka daraja Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za Kikwajuni, Mundu, pamoja na Miembeni, zimeshuka daraja rasmi kwa upande wa Kanda ya Unguja kwa msimu huu wa 2019/2020, licha ya baadhi ya timu hizo kubakiwa na mchezo mmoja.

Kwa mantiki hiyo, msimu ujao wa 2020/21, sasa vigogo hivyo vya soka visiwani hapa, vitashiriki Ligi za Mikoa Kanda ya Unguja kuwania kurejea Ligi Daraja la Kwanza.

Timu ya Kikwajuni ambayo tayari imemaliza ligi hiyo, imefikisha alama 18 tu, huku Mundu yenye alama 19 bado ina michezo miwili kabla ya kumaliza ligi hiyo wakati Miembeni imefikisha alama 20 huku ikibakiza mchezo mmoja.

Timu moja ambayo imebaki kuungana na timu hizo tatu ili kutimia nne zitakazoshuka daraja msimu huu kwa Kanda ya Unguja ni kati ya Bweleo ambayo ina alama 27, huku ikiwa tayari ishamaliza ligi na timu ya Kilimani City ambayo ina alama 26, huku ikiwa imebakiwa na mchezo mmoja, hivyo endapo itashinda mechi yake ya mwisho itajinusuru na janga hilo la kushuka daraja.

## Waluguru Original wakataa wanaume

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya muziki wa dansi ya Waluguru Original ya mjini Morogoro, imesema haina mpango na wanenguaji wa kiume, kwa madai kwamba kwa mazingira ya muziki wameshapitwa na wakati.

Mkurugenzi wa Waluguru Original, Killer Man, alimwambia mwandishi wetu jana kuwa, tangu aanzishe bendi hiyo mwaka 2014, haijawahi kuwa na mnenguaji wa kiume bali wa kike tu ambao ni burudani tosha kwa mashabiki wa muziki wa dansi.

"Wanenguaji wa kiume walikuwa na umuhimu zamani, lakini leo mashabiki wanatamani kuwaona wa kike wakifanya vitu vyao, ndiyo maana katika bendi yetu wapo wa kike tu," alisema Killer Man.

Alisema, Waluguru Orignal inafanya kile ambacho mashabiki wanakitaka ili mradi kiwe na manufaa kwa pande zote ikiwamo kuwa na wanenguaji wa kike tu ambao wamechangia kuifanya bendi hiyo kuwa maarufu.

# KINARA WA MABAO LIGI KUU Z'BAR ATUA MTIBWA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MTIBWA Sugar imefanikiwa kuinasa saini ya kinara wa mabao Ligi Kuu Zanzibar, Ibrahim Hamad Ahmada Hilika, kutoka Klabu ya Zimamoto ya visiwani hapa kwa mkataba wa miaka miwili, imeelezwa.

Hilika ambaye anaichezea timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), msimu uliopita wa Ligi Kuu Zanzibar 2019/20, alitwaa Kiatu cha Dhahabu baada ya kupachika kimyani mabao 20 kwenye ligi hiyo iliyoshirikisha timu 16, huku Mlandege ikitwaa ubingwa na timu yake ya Zimamoto ikimaliza nafasi ya pili.

**Akizungumza na gazeti hili jana, alisema malengo yake makubwa yalikuwa ni kuona siku moja anacheza ligi yenye ushindani zaidi nje ya Zanzibar, ili kujiendeleza kisoka kupitia nafasi yake ya ushambuliaji anayocheza.**

Alisema Wazanzibar pamoja na mashabiki wake waliopo visiwani hapa, watarajie mambo mazuri katika timu yake mpya ya Mtibwa Sugar ambayo anaamini malengo yake ya kuwa mshambuliaji hodari yanaenda kutimia kutokana na timu anazoenda kukutana nazo katika Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa na wachezaji wenye uzoefu mkubwa kisoka.

"Ninajua Ligi Kuu Bara ina ushindani mkubwa kulingana na wachezaji wa timu mbalimbali wanaosajiliwa kuzitumikia wakiwamo wa kigeni, hivyo kwa upande wangu nimejipanga kuhakikisha naitumia vema nafasi niliyoipata kwa kuwa tayari nina uzoefu wa kucheza mashindano tofauti," alisema.

NAKUTOKA...



Kiungo wa Mtibwa Sugar, Haroun Chanongo, akimtoka beki wa Kagera Sugar katika mchezo wa kirafiki kujiandaa na msimu mpya uliopigwa katika Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro jana na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DStv yazindua msimu mpya wa soka

**Na Mwandishi Wetu**

SUPERSPORT ambayo ni maarufu kwa kurusha mubashara michezo mbalimbali duniani imetangaza kuzinduliwa rasmi kwa msimu wa soka, ambapo sasa maandalizi ya ligi kubwa na maarufu duniani yamekamilika na ligi hizo zitaanza siku si nyingi.

Kwa upande wa Tanzania uzinduzi huo ulifanyika jijini Dar es Salaam jana na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa soka wakiwamo wachezaji wakongwe waliocheza Ligi Kuu Tanzania pamoja na timu ya Taifa, 'Taifa Stars' kwa miaka mingi.

Akizungumza katika hafla hiyo Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo alisema DStv kwa kupitia chaneli za SuperSport kama kawaida yake msimu huu watawaletea Watanzania burudani hiyo mubashara na kwamba tofauti na miaka iliyopita, msimu huu chaneli za SuperSport zimepangwa upya kulingana na aina ya mchezo unaoonyeshwa.

"Safari hii DStv na SuperSport tunakuletea 'Soka Lisilopimika!' Tumejipanga vizuri zaidi na mbali ya kukuletea michuano mikubwa duniani kama Ligi Kuu ya England (EPL), Ligi Kuu ya Hispania (La Liga) na nyinginezo, sasa chaneli za SuperSport zimepangwa mahususi kulingana na aina ya mchezo unaoonyeshwa. Kwa msingi huo, sasa kutakuwa na chaneli mahusus kwa ajili ya Ligi Kuu England, chaneli mahususi kwa Ligi ya Hispania, chaneli mahususi kwa Ligi ya Italia (Serie A) na kadhalika," alisema Shelukindo.

Alisema mbali na ligi hizo tatu kubwa duniani, SuperSport itaendelea kuonyesha mashindano mengine makubwa kama Euro 2020 Championship, Kufuzu UEFA Euro 2020, kuwania Kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar kwa timu za Ulaya, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Mataifa ya Ulaya.

"Mwaka huu kwa kweli kutakuwa na burudani ya aina yake ndani ya DStv na mipango tayari imeshakamilika na punde tu hali itakaporuhusu tutaanza kurusha ligi hizo kubwa kwa lugha ya Kiswahili kupitia SuperSport," alisisitiza Shelukindo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa hafla hiyo wachezaji wakongwe hapa nchini akiwamo Edibily Lunyamila, Fikiri Magoso, Mohammed Mwameja, Madata Lubigisa na wengineo, walisema wakati umefika kwa Watanzania kujifunza kutoka kwa wenzetu ambao wako juu kisoka ili na Tanzania iweze kufikia viwango hivyo.

Walisema kuonekana kwa ligi kubwa duniani mubashara hapa nchini, kuwe chachu ya kujifunza kutoka kwa wenzetu ili kuimarisha soka la Tanzania na hatimaye liwe katika viwango kama walivyofikia wao.

Kutokana na kuchelewa kukamilika kwa msimu uliopita, ligi hizo maarufu duniani - Premier League, LaLiga na Serie A zitaanza mwezi ujao ambapo Ligi Kuu England na Hispania zitaanza Septemba 12 wakati ile ya Italia ikianza wiki moja baadaye.

Ligi Kuu England itashuhudiwa ujio wa timu mpya zilizopanda kama Leeds United, West Bromwich Albion na Fulham wakati kule Italia, Benevento na Crotone nazo zimepanda daraja. Kwa upande wa LaLiga, Cadiz na Huesca ni ingizo jipya kwenye ligi hiyo msimu huu.

Michezo
Alhamisi Agosti 27, 2020
Nipashe



Messi aomba rasmi kutimka Barca UKURASA 22

NDIO ZANGU...



Mshambuliaji wa Simba, Bernard Morison, akifanya vitu vyake wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 5-2 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Transit Camp iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sven autaja mfumo mpya Simba 2020/21

## ● ● ● Asema hana namna zaidi ya kwenda na mifumo miwili tofauti na kuachana na 4:2:3:1 ili...

**Na Saada Akida**

HUKU akishuhudia timu yake ikishinda mechi mbili tofauti za kirafiki kwa siku moja katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana ikiwa na nyota wake wapya, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbreock ametikisa kichwa na kisha kusema "msimu huu huenda nikabadilisha mfumo kutoka mmoja niliokuwa nikiutumia na kwenda na miwili."

**Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi mbili za kirafiki Simba iliyocheza dhidi ya KMC FC na kushinda 3-1, kisha kuingiza kikosi kingine katika mchezo wa pili na kushinda 5-2 dhidi ya Transit Camp, Sven alisema atalazimika sasa kuachana na mfumo wake wa 4:2:3:1 aliotumia msimu uliopita.**

Sven alisema kutokana na ubora wa wachezaji alionao katika kila nafasi uliochangiwa na nyota wapya ambao wameongeza ushindani wa namba kuelekea msimu mpya wa 2020/21, sasa atatumia mifumo miwili ambayo ni 4:4:2 na 4:3:3, ambayo anaamini itamwezesha kufikia malengo yake ya kuendelea kutwaa mataji.

"Katika mifumo hiyo, nitaangalia jinsi wachezaji wangu watakavyoweza kwenda nayo vizuri, lakini mpinzani wangu ambaye nashindana naye," alisema kocha huyo.

Alisema wanatarajia kuondoka kesho (Ijumaa), kuelekea Arusha tayari kwa mechi yao ya Ngao ya Jamii dhidi ya Namungo FC itakayopigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini humo.

"Timu imekuwa vizuri hasa katika hizi mechi tatu za kirafiki ambazo zimenipa mwanga wa kuona mapungufu ya kikosi changu na kufanyia kazi kuelekea mchezo wetu dhidi ya Namungo," alisema Sven.

Alisema kwa kikosi alichonacho msimu huu, ni bora zaidi, kwa kuwa maingizo mapya ya wachezaji yanampa uhakika wa kuchezesha vikosi viwili vya ushindani na kupata matokeo.

"Namungo ni timu nzuri na kila mmoja amejipanga vizuri kuhakikisha tunaonyesha mpira mzuri, nitaondoka na wachezaji 27, nitawakosa Chris Mugalu ambaye aliondoka kwenda kwao (DR Congo) kuweka mambo yake sawa kabla ya kurejea kufanya kazi rasmi pamoja na Gerson Fraga (aliyekwenda kwao Brazil kwa matatizo ya kifamilia)," alisema kocha huyo.

Kuhusu wachezaji wawili ambao hawajaungana na wenzao, Pascal Wawa aliyetarajiwa kuwasili jana na Luis Miquissone anayewasili kesho, alisema hawatakuwapo katika program ya mchezo huo.

Katika mechi ya kwanza jana dhidi ya KMC, Simba iliwachezesha Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein, Kennedy Juma, Joash Onyango, Jonas Mkude, Mzamiru Yassin, Clatous Chama, John Bocco, Ibrahim Ajibu na Miraji Athumani. Mabao katika mechi hiyo yalifungwa na Chama, Ajibu na Mzamiru huku la KMC likifungwa na Ralient Lusajo.

Mechi ya pili dhidi ya Transit Camp, Simba iliwachezesha Beno Kakolanya, Gadiel Michael, David Kameta, Erasto Nyoni, Ame Ibrahim, Said Ndemla, Rally Bwalya, Bernard Morrison, Cyprian Kipenye, Meddie Kagere na Charles Ilamfya. Wafungaji wa mabao walikuwa Kipenye (mawili dakika ya pili na 26) Ilamfya (dk. 17), Kagere (dk. 44) huku Gadiel Michael akitupia la mwisho dakika ya 71, wakati yale ya wapinzani yote yakifungwa na Iddi Mbaga.

Hata hivyo, mechi ya pili ilimalizika zikiwa zimesalia dakika tano kabla ya kipenga cha mwisho baada ya Sven kuamuru refa amalize kutokana na kukerwa na rafu aliyochezewa Bwalya na Kipenye, lakini alieleza hawakupata majeraha makubwa.

# Cedric atoa sababu kuitosa Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wa Yanga wakitarajia kumpokea Kocha Mkuu, Cedric Kaze, aliyeelezwa kwamba angetua keshokutwa, Ijumaa tayari kwa kukinoa kikosi hicho kuelekea msimu mpya wa 2020/21, hatimaye ameota mbawa, imeelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa zilizolifikia Nipashe jana muda mfupi kabla ya kuelekea mitamboni, zilieleza kuwa Cedric amekataa ofa hiyo huku akitoa sababu kwamba ana matatizo ya kifamilia.

Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Fredrick Mwakalebela, alipoulizwa kuhusu suala hilo, alisema ni kweli ana matatizo ya kifamilia na wapo kwenye kikao cha kuamua nani apewe mikoba ya ukocha, kumrithi Mbelgiji Luc Eymael aliyetimuliwa mwishoni mwa msimu.

"Ni kweli kocha ana matatizo ya kifamilia, jioni hii (jana jioni) kuna kikao kinaendelea kuona nani apewe mikoba hiyo," alisema Mwakalebela.

Hata hivyo, chanzo chetu kingine kutoka ndani ya Kamati ya Usajili, kilitueleza jopo hilo lilikuwa likipitia rundo la CV (wasifu) za makocha wengine ambao waliomba kazi hiyo, hivyo mashabiki watarajie kutangaziwa kocha mwingine mapema iwezekanavyo.

Yanga ambayo imefanya usajili makini katika dirisha hili linalotarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi huu, kikosi cha timu hiyo kinaendelea na mazoezi chini ya Kocha wa viungo, Riedoh Berdien akisaidiana na mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo, Said Maulid 'SMG'.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >